NEWS @ The Foundation

ISSN 1821 - 5335 Toleo Namba 42 Jarida la Foundation for Civil Society Machi 2017

FCS yaalika wadau kutuma maombi ya ruzuku

Wafanyakazi wa FCS wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kusherehekea Siku ya Kimataifa ya Wanawake kwa kusikiliza historia binafsi ya maisha ya Bi. Angela Benedict (wa tisa toka kushoto), ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wote Sawa.

Shirika la Foundation for Civil Society (FCS) limetoa wito kwa Taasisi za Kiraia (za Tanzania Bara, Unguja na Pemba) kutuma maombi ya kupatiwa ruzuku kwa ajili ya kutekeleza miradi katika tasnia ya Utawala Bora.

Msingi wa ruzuku hii ya FCS unasimama katika dhana kwamba, utawala bora kwa umma husaidia kukuza uchumi na mshikamano wa kijamii, kupunguza umaskini na kuboresha mazingira endelevu. Miradi pia inalenga kuongeza imani ya wananchi kwa serikali kwa kuwa pasipokuwa na mshikamano na wananchi wenye kupaza sauti zao, upo uwezekano wa hali ya uchumi kuzorota.

Pia, pale ambapo umaskini na ukosefu wa usawa vinaposhamiri katika jamii kunapunguza ushiriki

Inaendelea Uk. 2

Kwa Mawasiliano:
Foundation for Civil Society
Mtaa wa Madai Cresent, 7 Ada Estate
Kitalu Na. 154.
S.L.P. 7192 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255-22-2664890-2
Nukushi: +255-22-2664893
Barua pepe: information@thefoundation-tz.org
Tovuti: www.thefoundation.or.tz

"Foundation News" ni jarida linalotolewa na FCS kwa lengo la kupashana habari juu ya shughuli zake na zile za sekta ya Asasi za Kiraia Tanzania.

YALIYOMO NDANI..

Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji Uk. 2

DANIDA yaipa FCS bilioni 12. 7 Uk. 3

Uelewa wa Watu wenye Ulemavu waongezeka Uk. 5

Marekebisho ya Dhana ya Mabadiliko ya FCS Uk. 9

Asasi zapambana na unyanyapaa wa Watu Wenye Ulemavu Biharamulo Uk. 11

UKaid from the British people
TRADE MARK EAST AFRICA Growing Prosperity Through Trade
Swiss Agency for Development and Cooperation SDC
EMBASSY OF DENMARK DANIDA
Norad

Ujumbe wa Mkurugenzi Mtendaji

Francis Kiwanga
Mkurugenzi Mtendaji
fkiwanga@thefoundation-tz.org

Kwa mara nyingine, nawaalika kulisoma Jarida la FCS ambalo ni la kwanza kwa mwaka 2017. Kwa kuzingatia kuwa hili ni toleo la kwanza kwa huu, natumaini kuwa mtakuwa na shauku kubwa ya kupata taarifa zilizomo katika chapisho hili. Taarifa kuhusu utendaji wa FCS kama ulivyoainishwa ndani ya toleo hili, pia zinajumuisha shughuli za wadau wetu wakuu, ambao ni Asasi za Kiraia zilizopo nchini.

Kwenye robo ya kwanza ya mwaka 2017, FCS tulitafakari utendaji wetu. Tulitathmini jinsi tunavyosimama hivi sasa, na ipi itakuwa nafasi yetu siku zijazo. Aidha, tuliangalia upya na kutilia mkazo njia zinazoweza kulifanya shirika letu liwe mfano wa uwazi katika utoaji ruzuku.

Ili kulifikia lengo letu, tulifanikiwa kupata msaada wa Shirika la INTRAC, ambalo lilitusaidia kuitathmini Dhana ya Mabadiliko na hivyo kuimarisha Mfumo Wetu wa Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo na kulifanya shirika kuchangia mawazo yahusuyo utendaji na jinsi tunavyotaka vigezo vyetu viendane na mitizamo chanya ya wadau wetu.

Natumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi ya Wakurugenzi wa FCS kwa ushiriki wake katika kuipitia upya Dhana ya Mabadiliko.

Natumia pia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Washirika wetu wa Maendeleo ambao walishiriki kwenye zoezi hili mwanzo hadi mwisho. Sisi wa FCS tunawashukuru sana kwa kutuwezesha kufanikisha kusudio letu la kuwa na Dhana ya Mabadiliko, ambayo itaitofautisha FCS na mashirika mengine, kwani dhana hiyo itatuwezesha kuboresha utendaji wetu wa kila siku.

Nitumie fursa hii kuwaarifu kwamba mabadiliko tunayoanzisha yanalenga kuboresha utendaji wetu ili kupata matokeo mazuri tukizingatia suala zima la Utawala Bora jambo ambalo linajumuisha masuala yote mtambuka. Eneo hili linahitaji mfumo imara, ambao ni rahisi na unaoweza kurekebishwa, kwa lengo la kuimarisha zaidi. Pindi unapokuwa na mfumo kama huo, mchakato mzima wa kuleta mabadiliko unakuwa rahisi na endelevu.

Natumia pia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Washirika wetu wa Maendeleo ambao walishiriki kwenye zoezi hili mwanzo hadi mwisho. Sisi wa FCS tunawashukuru sana kwa kutuwezesha kufanikisha kusudio letu la kuwa na Dhana ya Mabadiliko, ambayo itaitofautisha FCS na mashirika mengine, kwani dhana hiyo itatuwezesha kuboresha utendaji wetu wa kila siku.

Kuelekea mwisho wa mwaka 2016, rafiki zetu wa DANIDA walikubali kushirikiana nasi kuanzia mwaka huu hadi mwaka 2021. Hii ni faraja kubwa kwetu inayotupa changamoto ya kuzidisha matokeo yetu kuliko yale tuliyokwisha pata. Tunawashukuru kwa makubaliano hayo, pia tunaendelea kuwashukuru pia Washirika wetu wengine wa Maendeleo.

Natoa wito kwa asasi zitakazoomba ruzuku mwaka huu kuwasilisha maombi yao kwa wakati. Ni matumaini yangu kwamba watadhihirisha ubunifu bora kabisa katika kuandaa maombi ya miradi yao.

Maombi ya Fedha za Miradi sharti yazingatie utekelezaji wa mipango ya utawala bora nchini Tanzania. Mpango wetu wa Utawala Bora umebuniwa kwa kuzingatia uwepo wa fungamano imara lenye changamoto baina ya umaskini, matabaka ya watu na utawala. Tafadhali itumieni fursa hii ili kuisaidia jamii yetu kusonga mbele katika masuala ya maendeleo.

Niwatakie usomaji mwema na wenye mafanikio katika kuiimarisha sekta ya Asasi za Kiraia.

FCS yaalika...

Kutoka Uk. 1

wa wananchi, hutishia amani na kuishi kwa umoja, hudhoofisha mchakato wa kisiasa na hutengeneza uongozi wenye mapungufu.

Utoaji wa ruzuku kwa mwaka huu utazingatia aina mbili za matokeo, yaani (i) Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma bora zaidi na (ii) Mchakato wa kufanya maamuzi ya kisiasa ili kuimarisha haki za wananchi, hasa za makundi yaliyotengwa wakiwemo Watu Wenye Ulemavu, makabila madogo na wanawake.

Waombaji wa ruzuku kwa ajili ya matokeo yahusuyo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitoe kutoa huduma bora zaidi wanapaswa kuwasilisha mapendekezo ya miradi inayohusiana na miradi ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa Kijamii na Ufuatiliaji wa Matumizi ya Serikali.

Waombaji wa kundi hili wawe wanaofanya shughuli zao katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Manyara, Tanga na Morogoro, mkazo utawekwa kwenye miradi ya elimu. Mikoa mingine ni: Kilimanjaro, Dar es Salaam na Tanga (sekta ya maji), Morogoro, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Songwe (kilimo).

Kwa mikoa ya Kigoma, Geita, Kagera, Mwanza na Singida, msisitizo utakuwa kuupa nguvu ushiriki wa wananchi kwenye mipango ya umma (upangaji na ugawaji wa rasilimali), vilevile utoaji wa taarifa za matumizi ya rasilimali au usimamizi kwenye ngazi za mitaa na za kitaifa.

Kwenye matokeo ya pili, yanayojumuisha utoaji wa maamuzi na ukuzaji demokrasia ambao unalenga haki za wananchi hasa katika makundi yanayotengwa, Watu wenye Ulemavu, makabila madogomadogo na wanawake FCS inakaribisha maombi kutoka Asasi za Kiraia zitakazotekeleza miradi kwenye maeneo yafuatayo: Uundaji wa majukwaa ya vijana katika ngazi ya wilaya ili kuongeza sauti za vijana na ushiriki wao kwenye uendelezaji wa Sera ya Maendeleo ya umma na utekelezaji wake. Mikoa itakayohusika na lengo hili ni: Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Zanzibar (Pemba na Unguja) Dodoma, Tanga na Mbeya. Kwenye lengo la Utetezi dhidi ya mila haribifu mikoa itakayohusika ni: Arusha, Shinyanga, Simiyu, Mtwara, Manyara, Kilimanjaro, Dodoma, Singida na Mara.

Miradi ya kampeni na utetezi dhidi ya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) itahusisha mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Geita, Katavi, Simiyu, Tabora na Rukwa.

Kuhusu utetezi wa haki za Watu Wenye Ulemavu na kuongeza ushiriki wao katika uwajibikaji kwenye shughuli za umma na katika serikali za mitaa, mikoa yote ya Tanzania itahusika.

Katika eneo la uhamasishaji wa upatikanaji wa ardhi na haki nyingine za umiliki, hasa kwa wanawake asasi kutoka mikoa ya Arusha (Arumeru), Manyara (Kiteto) Morogoro na Iringa zitahusika. FCS inatarajia kutoa ruzuku kwa asasi 150, ambazo maombi yao yatakidhi vigezo.

MAOMBI YA WATU WENYE ULEMAVU

Mwezi Februari mwaka huu, FCS ilitoa wito kwa Asasi za Watu Wenye Ulemavu kutuma maombi kwa ajili ya kupata ruzuku zinazolenga kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu kwenye sekta za afya na elimu. FCS ilipokea maombi 123. Baada ya upembuzi, asasi 10 zimepitishwa kupokea ruzuku hizo.

DANIDA yaipa FCS bilioni 12.7

Serikali ya Denmark, kupitia Shirika lake la Kimataifa la Maendeleo, DANIDA, imeingia mkataba na Foundation for Civil Society (FCS) ambapo serikali hiyo itatoa DDK 40 milioni (sawa na Tsh. Bilioni 12.7) kama msaada kwa kipindi cha miaka sita.

Uwekaji wa sahihi ulifanyika kwenye Ubalozi wa Denmark Jijini Dar es Salaam. Mheshimiwa Eirnar Jensen, Balozi wa Denmark nchini Tanzania, aliweka sahihi kwa niaba ya DANIDA, ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Wakili Francis Kiwanga, aliweka sahihi kwa niaba ya FCS. Akizungumzia baada ya zoezi la kuweka sahihi kwenye mkataba Bw. Kiwanga alisema ilikuwa heshima kubwa kwa FCS kupokea ruzuku hiyo ambayo itachangia kwenye utekelezaji wa Mpango Mkakati wa mwaka 2016 -2020.

"Tunatambua jukumu letu la kuziunga mkono asasi za kiraia nchini Tanzania. Tunayo sifa njema ya kushughulikia masuala ya utawala bora," alisema Bw. Kiwanga, huku akidhihirisha hamu ya FCS kuziunga mkono asasi za kiraia zinazojihusisha na masuala ya utawala bora nchini Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Bw. Francis Kiwanga, akiweka sahihi kwenye mkataba wa ruzuku baina ya Foundation na Balozi wa Denmark nchini Tanzania, Mheshimiwa Eirnar Jensen.

Utoaji wa ruzuku hiyo ni matokeo ya vifungu vya jumla vya makubaliano baina ya Denmark na Tanzania kuhusu ushirikiano wa maendeleo katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tanzania wa mwaka 2014-2019 na Programu ya 2016-2021 ya Utawala na Haki za Binadamu.

Lengo la makubaliano haya ni kukuza utawala bora, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu. Kwa njia ya ruzuku hii, FCS itayaongezea nguvu mafanikio chanya yaliyopatikana kwenye masuala ya utawala bora, uwajibikaji wa umma na umoja wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hasa kwenye ngazi za chini, pamoja na kuendelea kuimarisha asasi za kiraia na muungano wa Azaki hizo.

Msaada huu utachangia kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME), yaani kukuza jamii zinazoshirikiana zenye amani na umoja; kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu, kuwezesha upatikanaji wa haki kwa wote na ujenzi wa taasisi zenye ufanisi, uwajibikaji jumuishi katika ngazi zote (MME 16). Lengo la pili ni kufikia usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake na wasichana (MME 5).

Uimara Serikali za Mitaa kuimarisha utawala bora Kagera

Iwapo Serikali Kuu haitaziimarisha Serikali za Mitaa ili ziweze kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa maamuzi, upangaji wa miradi na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma, hasa katika maeneo ya vijijini, upo uwezekano wa maeneo ya vijijini kuwa na maendeleo duni.

Maelezo haya yameelezwa na viongozi wa Asasi ya Kagera Development and Credit Revolving Fund kwa kifupi KADETFU, ambayo ni asasi ya kiraia inayofadhiliwa na FCS.

Viongozi wa KADETFU walitamka hivyo walipotoa maelezo kwa FCS kuhusu matokeo ya mradi wa majaribio unaotekelezwa hivi sasa, unaojulikana kwa jina la Mradi wa Kujenga Uwezo wa Viongozi wa Umma, Vijiji na Kata kwenye Upangaji Shirikishi wa Mchakato wa Bajeti na Maendeleo kwenye Wilaya ya Bukoba.

Syliveter Busanya, Mratibu wa Mradi wa KADETFU, alisema shirika hilo, ambalo lengo lake ni kulinda haki za binadamu, uhifadhi wa mazingira, uwezeshaji na uendelezaji wa kijamii, kiuchumi, na maendeleo ya utamaduni; linaiwezesha jamii kuandaa na kupigania mahitaji yao kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao. Hadi hivi sasa, mradi huo umevifikia vijiji 11 vya wilaya ya Bukoba.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Miradi, wanavijiji hawana uelewa kuhusu masuala ya haki zao, hasa katika kuwawajibisha viongozi. Vilevile, kamati za maendeleo za kata zilionekana kuwa na ufahamu mdogo wa majukumu yao.

Alisema kutokana na kuwa na uelewa mdogo, wanavijiji hunyimwa haki yao ya uraia ya kushiriki kwenye uanzishaji wa miradi na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyopo kwenye maeneo yao.

Kwenye baadhi ya maeneo, KADETFU ilibaini kutokuwepo kwa mikutano ya mabaraza ya vijiji, hali ambayo iliathiri masuala ya maendeleo ya vijiji, kama vile utoaji wa maamuzi juu ya Mpango wa Matumizi ya Mpango Ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

"Iwapo serikali inataka kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi zinatumika vema, basi inahitaji kuwekeza katika kujenga uwezo kwenye ngazi za chini," Mratibu alisisitiza na kuongeza:

"Sisi katika KADETFU, kutokana na ruzuku kutoka kwa FCS, tumepata matokeo ya kuridhisha kwenye maeneo tuliyoyatembelea hadi hivi sasa. Wakati wa kutekeleza jukumu hili, tumegundua kwamba kuna haja kubwa kwa serikali kushirikiana na asasi za kiraia ili kujenga uwezo wa wananchi kwenye ngazi za mitaa kwa ajili ya kuimarisha utawala bora," alisema.

Agastin Angelo, ambaye pia anafanya kazi na KADETFU alisema kwenye maeneo yaliyotembelewa na KADETFU wanakijiji walikuwa na uwezo wa kuwabana viongozi wa vijiji ili waitishe vikao, ambapo waliwataka viongozi hao kujibu hoja mbalimbali.

Kwa mujibu wa Angelo, kutokana na ruzuku iliyotolewa na FCS, KADETFU inawafundisha wajumbe wa kamati za maendeleo za vijiji na kata ili wazingatie majukumu ya kila kikundi kulingana na matakwa ya utawala bora.

"Ingawa FCS kupitia asasi za kiraia kwa wakati wote imekuwa chachu ya kujenga uwezo wa asasi za kiraia hapa nchini, tunafikiri kuwa ni shurti pia ielekeze rasilimali zake kwenye mashina ili wananchi waweze kushiriki kwenye maamuzi, kufuatilia matumizi ya fedha za umma pia uwajibikaji wa viongozi wao," alisema.

FCS, KADEFTU ilivyowahamasisha viongozi

Viongozi wa serikali za mitaa katika wilaya ya Bukoba Vijijini wameonyesha furaha yao baada ya kupewa mafunzo ya uongozi. Wakiongea baada ya kuhudhuria semina, walikiri kuwa utendaji wao wa kazi umekuwa rahisi zaidi na wenye mafanikio kuliko ulivyokuwa hapo zamani.

Wakisimulia jinsi mafunzo yalivyowasaidia kubaini namna ya kuongoza kwa kufuata misingi ya utawala bora, viongozi wa serikali za mitaa wa vijiji viwili kati ya 11, ambao walitembelewa na maofisa wa Mfuko wa Maendeleo na Mikopo Kagera (Kagera Development and Credit Revolving Fund), kwa kifupi KADETFU, walikiri kuwa utendaji wao umebadilika na kwamba wanavijiji wanaitikia vema na wanashiriki kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo.

KADETFU iliendesha awamu ya kwanza ya mafunzo kwenye vijiji 11 kama sehemu ya mradi wa "Kujenga Uwezo wa Viongozi wa Umma, Vijiji na Kata katika Mipango Shirikishi na Mchakato wa Bajeti kwenye Wilaya ya Bukoba." Mradi huo umewezeshwa na msaada wa kifedha uliotolewa na FCS.

Kwa mujibu wa viongozi wa serikali za mitaa, hivi sasa, wanawashirikisha kikamilifu wanakijiji kutoa maamuzi kwa kuitisha mikutano, jambo ambalo hapo awali halikuwapo. Alisema kuwa wao, kama viongozi wa mitaa, hawakabiliwi tena na mfumo wa utawala wa kutoka juu kama ilivyokuwa hapo awali.

Yafuatayo ni maelezo ya walionufaika na mafunzo:

Meliciana Morice (Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji cha Karonge)

Namshukuru Mungu kwa kunipatia fursa ya mafunzo. Kabla ya mafunzo, nilikuwa sielewi kabisa nafasi yangu kama mjumbe wa kamati ya maendeleo ya kijiji. Sasa naelewa jinsi ya kuwahusisha wanakijiji wenzangu katika kufanya maamuzi pindi suala lolote linapojitokeza.

Sweetbert Pontian (Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji cha Karonge)

Mafunzo haya yamejenga uwezo wangu wa kuongoza. Hivi sasa naelewa mipaka ya majukumu na wajibu wangu. Wakufunzi wametuhamasisha kuhusu umuhimu wa kuitisha mikutano ya kijiji kwa ajili ya kujadili masuala ya maendeleo na kuwapa wananchi fursa ya kutoa maoni yao.

Nafahamu pia kwamba wananchi ndio wenye jukumu la kuanzisha miradi itakayotekelezwa. Mradi wowote unapopendekezwa na mamlaka za wilaya, tunaitisha kikao cha wanakijiji ili kujadili ustahiki wake. Hatutekelezi mambo tuliyoletewa kutoka ngazi za juu bila kuyachekecha.

Theotestina Michael (Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Bundaza)

Baada ya kupata mafunzo, hivi sasa tunaitisha vikao vya kijiji ambapo wanavijiji wanahoji mambo mbalimbali nasi tunawapatia majibu.

Bonaventura Ndibalema (Mwenyekiti wa Kijiji cha Bundara)

Mafunzo yamepanua uelewa wa majukumu yetu. Kabla ya kupata mafunzo, tuliendesha shughuli zetu kienyeji. Tunamshukuru mambo yamebadilika hivi sasa. Warsha imetufungua macho kuhusu masuala ya utawala bora. Mafunzo haya yametufumbua macho kuhusu suala la utawala bora. Wakufunzi walitufundisha jinsi ya kuanzisha miradi, pamoja na njia ya kubuni mpango wa utekelezaji kabla ya kuanzisha mradi wowote.

Bruno Kahwa (Afisa Mtendaji Kijiji cha Karonge)

Nawashukuru kwa dhati wote waliowezesha kuanzishwa kwa mafunzo haya. Baada ya kuhudhuria semina, nimetambua kuwa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji wamebadili sana mtazamo wao.

Kazi yangu imekuwa rahisi zaidi kwa kuwa sasa wajumbe wa kamati ya maendeleo ya kijiji na wanakijiji wanayafahamu majukumu yao. Uelewa huo umewawezesha wanakijiji kudai majibu sahihi kutoka kwetu au pale viongozi wa ngazi za juu zaidi wanapotutembelea. Tunaishukuru KADETFU kwa dhati na wale wote waliofanikisha semina. Tunachoomba ni mafunzo zaidi.

Winifrida Bonaventura (Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji cha Bundaza)

Mimi binafsi naishukuru KADETFU kwa mafunzo niliyopata. Hivi sasa niko karibu zaidi na wanakijiji wenzangu. Pale ambapo wanadai majibu kuhusu masuala mbalimbali, nawajibu inavyotakiwa. Mafunzo haya yameongeza ujasiri kwa wanawake.

Wanawake walizoea kutohudhuria mikutano, walipohudhuria hawakuuliza maswali au kutoa maoni yao kwenye hadhara. Hivi sasa wanaomba nafasi za kuuliza maswali na kisha wanachangia kwenye majadiliano. Mafunzo yametusaidia pia kujua kuwa tunao wajibu wa kufahamu mipaka ya kijiji chetu. Hii imetusaidia kupata taarifa kuwa tuna mgogoro wa ardhi katika kijiji chetu baada ya baadhi ya watu binafsi waliopanda misonobari kwenye maeneo yaliyotengwa kama malisho kwa wafugaji.

Florence Baltazar (Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji cha Bundaza)

KADETFU imetufungua kuhusu masuala kadhaa ambayo hatukuwa na ufahamu wa kutosha. Hivi sasa tunajua kwamba ni muhimu tuifahamu mipaka ya maeneo yetu ya utawala na ya kijiji kizima. Kwa sasa, najua taratibu za kuitisha mikutano ya kijiji na kalenda ya mwaka mzima.

Selialis Josue (Mwenyekiti wa Kijiji cha Karonge)

Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuwania wadhifa wa Mwenyekiti wa Kijiji na kushinda uchaguzi mnamo mwaka 2014, niligundua kuwa mafunzo haya yalikuwa muhimu sana kwangu. Nilijifunza kuwa kuwashirikisha wananchi katika maamuzi muhimu lilikuwa jambo la lazima. Hicho ndicho tunachofanya sasa kwenye kijiji changu. Hakuna jambo linaloamuliwa bila kuwashirikisha wanakijiji.

Kwa maoni yangu, wafanyakazi wa KADETFU wametubadilisha kutoka kwenye mfumo mbovu wa uongozi hadi mtindo wa uongozi unaotokana na mfumo bora zaidi. Tangu KADETFU walipotoa mafunzo, wanakijiji wanahoji mambo. Wanadai majibu sahihi kwa masuala yanayojitokeza. Hivi sasa, wanawake wamepata ujasiri wa kuuliza maswali na kuzungumza hadharani kwenye mikutano ya hadhara.

Editha Johakim (Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji) Sikuwa nafahamu

umuhimu wa kuwahusisha wanakijiji kwenye kufanya maamuzi ya masuala yanayogusa maisha yao. Tulizoea kuamua kila jambo kwa niaba yao. Semina imenisaidia kuelewa ukomo na mipaka ya kazi yangu kama mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kijiji. Hivi sasa, mambo yanakwenda vema.

Mbinga: Uelewa wa Watu wenye Ulemavu waongezeka

Miongoni mwa makundi yenye haja kubwa ya kuwezeshwa, ambayo yanatengwa na jamii, ni watu wenye ulemavu. Foundation for Civil Society (FCS) inasaidia sana juhudi za makusudi za kuyashawishi Mashirika ya Watu wenye Ulemavu kutuma maombi ya ruzuku.

Mojawapo ya mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyopata ruzuku ya FCS ni Chama Cha Walemavu Tanzania (CHAWATA), ambacho kina ofisi yake wilayani Mbinga. CHAWATA ina lengo la kuwafanya watu wenye ulemavu waielewe Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya 2010.

Mradi huo unatekelezwa kwenye kata za Ruanda na Mpepani. Lengo lake ni kuwafikia watu 100 wenye ulemavu katika Wilaya ya Mbinga, ambayo ina watu 2852 wenye ulemavu, kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya Mwaka 2012. Azma ya kuibua mradi huo katika Wilaya ya Mbinga inatokana na ukweli kwamba, idadi kubwa ya watoa huduma za afya hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu haki za watu wenye ulemavu. Hali hii imesababisha usumbufu kwa wagonjwa wenye ulemavu wa kimwili, pamoja na watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi.

CHAWATA imeanzisha mpango wa uhamasishaji na kuongeza uelewa, unaotekelezwa kwa njia ya mikutano inayowashirikisha viongozi wa vijiji na kata, watu maarufu, waalimu na wafanyakazi wa afya. Zaidi ya hayo, zaidi ya watu 13 wenye ulemavu wamepata mafunzo ya uhamasishaji yanayoweza kuwafanya wawe kichocheo kwa jamii.

Imaculata Mapunda ni mjumbe wa viti maalum kwenye kata ya Ruanda. Baada ya kuhudhuria mafunzo ya kuongeza ufahamu, aliandaa mikutano kwenye vijiji na maeneo jirani kama njia ya kuuelimisha umma juu ya haki za watu wenye ulemavu. "Baada ya kupata mafunzo, tuliunda makundi ya watu wenye ulemavu na vikundi vya wanaume na wanawake ambao si walemavu. Hii ilikuwa ni njia ya kuongeza uelewa wa jamii kuhusu Sheria ya Watu Wenye Ulemavu 2010," alisema Immaculata.

PISCCA yawaasa wanufaika kufanya kazi kwa bidii

Wanufaika wa Mradi wa Ubunifu wa Muungano wa Taasisi za Kiraia nchini Tanzania maarufu kwa jina la PISCCA wametakiwa kuongeza bidii ili kuyafikia malengo ya miradi yao.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu ya jinsi ya kutumia ruzuku toka PISCCA, Mkuu wa Ushirikiano na Masuala ya Utamaduni kwenye Ubalozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Bw. Phillippe Boncour, alisema uteuzi wa miradi inayofadhiliwa na PISCCA ulitokana na ushindani mkubwa hivyo akawataka wanufaika wa mradi huo kutekeleza miradi yao kama ilivyopangwa ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

"Mmepitia ushindani mkali. Hivi sasa mpo hapa. Ujumbe wangu kwenu ni kwamba mnatakiwa mfanye kazi kwa bidii kwa kuzingatia miradi yenu," alisema Bw. Boncour kisha akatoa pongezi kwa Foundation for Civil Society (FCS) kwa ushiriki na jitihada za kuwaunga mkono wanufaika wa PISSCA.

Meneja Miradi wa FCS, Bw. Fransis Uhadi, aliitumia fursa hiyo kutoa pongezi zake kwa taasisi sita zilizoteuliwa, huku akisisitiza kuwa, mafunzo yaliyotolewa na FCS ni muhimu kwa vile yanalenga kujenga uwezo wa kutumia mbinu bora katika usimamizi wa miradi.

Mkuu wa Ushirikiano na Masuala ya Utamaduni kwenye Ubalozi wa Ufaransa, Bw. Phillipe Boncour (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Bw. Francis Kiwanga (kushoto) wakati wa uwekaji sahihi wa mkataba wa PISCCA.

"Nawasihi mshiriki kwenye mafunzo haya kwa makini, ili mtakapoanza kutekeleza miradi yenu, mjaribu kuwa waangalifu kwenye usimamizi wa fedha kwa kuhakikisha uwepo wa uadilifu kwenye matumizi ya mradi," alisema.

FCS iliingia mkataba na Ubalozi wa Ufaransa wa kutoa mafunzo ya usimamizi wa ruzuku kwa asasi sita zilizonufaika na Mfuko wa Ubalozi wa Ufaransa kwa ajili ya Miradi Bunifu ya Asasi za Kiraia yaani PISCCA.

Mashirika yaliyonufaika na ruzuku hiyo ni: Friends of Lake Tanganyika (FOLT), Tanzania Climate Change Alliance (ZACCA), Tanzania Support for Women Rights (TASUWORI), Uigizaji Ngoma za Asili (UNA), White Orange Youth (WOY) na Medical Women in Tanzania(MEWATA).

Mafunzo hayo yalilenga kuboresha taarifa za miradi, hasa katika kuangalia matokeo tarajiwa na shughuli zilizobuniwa, ufuatiliaji wa miradi na usimamizi wa fedha. Kila shirika liliwakilishwa na washiriki wawili, mmoja mwenye uzoefu wa masuala ya fedha na mwingine mwenye ujuzi wa shughuli za miradi.

Jumla ya washiriki 12 (wanaume wanane na wanawake wanne) walihudhuria mafunzo hayo ya siku tatu yaliyofanyika katika hoteli ya Blue Pearl jijini Dar es Salaam. Yalianza Januari 12 hadi Februari 18.

Madiwani wapewa mafunzo ya afya Kyela

Mkuu wa Wilaya ya Kyela Claudia Kitha akifunga semina ya siku moja ya madiwani. Semina hiyo iliandaliwa na JTL na kuhudhuriwa na madiwani 45 wa Wilaya ya Kyela.

Jitambue Lembuka Tanzania (JTL), asasi ya kiraia iliyopo wilayani Kyela, imetoa mafunzo kwa madiwani 45 kuhusu changamoto zinazoikabili sekta ya afya katika wilaya hiyo. Mkurugenzi Mtendaji wa JTL, Bw. Simon Mkanya, alieleza kuwa mafunzo hayo yalifanikiwa na kwamba madiwani wilayani humo sasa wanatambua kuwa suala la afya linahitaji kupewa kipaumbele kwenye ajenda ya Halmashauri yao.

Bw. Mkanya alisema kuwa, Wilaya ya Kyela inakabiliwa na changamoto nyingi za afya ikiwa ni pamoja na vifaa duni vya afya. "Sisi tunafanya mradi wa utetezi wa afya katika Wilaya ya Kyela, ambao unafadhiliwa na shirika la Foundation for Civil Society (FCS). Tunaihamasisha jamii juu ya uelewa wa masuala ya afya,"alisema.

"Shirika la JTL huzingatia vitu vitatu, yaani mafunzo, ushauri wa kitaalamu na utetezi. Tumekuwa tukifanya hayo tangu mwaka 2008. Lengo letu ni kupanua huduma yetu katika Wilaya ya Kyela na kufikia watu wengi zaidi," alisema.

Mkanya alisema hapo awali JTL ilianzisha mradi wa kujenga uwezo wa ndani uliolenga uimarishaji wa taasisi yao ili iwe endelevu. "Chini ya mpango huo, tuliajiri wafanyakazi wenye mwelekeo unaofaana kubuni mpango wa muda mrefu ili kuyapa nguvu maono yetu, Tuliomba ruzuku kutoka FCS na kupokea shilingi milioni 40 ambazo zilitumika kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Ufuatiliaji wa Uwajibikaji Katika Jamii kwenye sekta ya afya. Fedha hii ilituwezesha kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya afya katika wilaya yetu," alisema.

Tumewafikia watu wengi wakiwemo madiwani. Tumewaelimisha njia bora ya kushughulikia huduma za afya," alisema na kuongeza; "mradi huu umeboresha uwezo wa wananchi na uwajibikaji kwenye wilaya. Sasa madiwani wametambua jukumu lao la kuboresha huduma za afya kwenye maeneo yao."

Bw. Mkanya alisema katika kutekeleza mradi huo, wafanyakazi hao wamepata ujuzi wa kina zaidi kuhusu mbinu za kuandaa maombi ya ruzuku na njia ya kutekeleza miradi ya Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa Jamii. Anasema kwamba mradi huu umewapa fursa ya kukua kama shirika na kujiimarisha kwenye maeneo ya utetezi kiasi ambacho wanaweza kutekeleza miradi mikubwa.

Alisema ukosefu wa ruzuku za kuendeshea miradi mingine ni changamoto kwa JTL. Suala hili linaizuia taasisi yao kutimiza lengo la kueneza shughuli zake kwenye wilaya nzima ya Kyela. "Tunayo ndoto kubwa ya kuipa nguvu jumuiya kwenye maeneo mengi. Hata hivyo, siyo rahisi kwetu kufika kila sehemu au kutekeleza sehemu kubwa ya mipango yetu," anasema.

Vilevile JTL inakusudia kuanzisha vituo vya elimu ya watu wazima katika Wilaya ya Kyela. Vituo tarajiwa vitatoa mafunzo na kuwezesha ubadilishanaji wa ujuzi kwenye maeneo kama huduma za afya, elimu na mazingira.

Madiwani wote 45 wa wilaya wamepata mafunzo ya ufahamu wa masuala ya afya yaliyotolewa na JTL, ambapo wameimarishwa kwenye eneo la utoaji wa huduma za afya. Zaidi ya hayo, wamekuwa na motisha ya kupigania ongezeko la bajeti ya afya kwa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

Kuna vijiji 37 tu ambavyo vinapata huduma ya afya kwenye Wilaya ya Kyela. Hii inamaanisha kwamba, watu wanaoishi kwenye vijiji vingine 60 wanalazimika kutembea umbali mrefu ili kupata huduma za afya.

MHNT yahamasisha vikao vya vijana mkoani Mbeya

Mbeya HIV/AIDS Network Tanzania (MHNT), ambayo ni asasi inayolenga kuleta uelewa juu ya VVU na UKIMWI, imezindua mpango maalum kwa ajili ya vijana. Kupitia mradi huo, vijana wanafundishwa kuhusu haki na majukumu yao katika jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa MHNT, Jonathan Mwashilindi anasema kwamba kutokana na ufadhili wa Foundation for Civil Society (FCS), wanatekeleza mradi kwenye kata tano. "Tumeanza kuutekeleza mradi mwaka jana. Tayari tumeshafanikisha mambo mengi. Tunayafikia makundi matano tofauti kwenye kata tano zilizoteuliwa. Tunawapa uelewa unaohitajiwa wa sera mbalimbali zinazowahusu vijana."

Mwashilindi anasema kwamba jukumu lao kubwa kama asasi ya kiraia ni kuwasaidia vijana kuanzisha vikundi ambavyo

Mwezeshaji anawafundisha vijana umuhimu wa kuunda majukwaa ya vijana. Tukio hili lilifanyika Mbeya, nalo liliandaliwa na MNHT.

vitakuwa majukwaa ya majadiliano na ushiriki. Wakati wa mikutano, vijana wa Mkoa wa Mbeya wanapata fursa ya kuzungumzia masuala yanayowagusa na kuyatafutia ufumbuzi.

"Pindi tutakapopokea fungu la pili la ruzuku, tutaharakisha utekelezaji wa mradi. Tutatilia mkazo suala la kuwasaidia vijana ili waweze kubuni miradi ya kiuchumi kwenye maeneo wanayoishi," anasema.

Inaendelea Uk. 7

UMATI yatoa wito kuwapatia ofisi masheha Zanzibar

Alli Suleiman (wa pili kushoto) anaeleza kuhusu shughuli za miradi yao kwenye ofisi kuu ya UMATI ya Unguja.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetakiwa kuboresha mahusiano baina ya wananchi na wawakilisi wao katika shehia. Shirika la Uzazi na Malezi Tanzania (UMATI), Tawi la Zanzibar, linaelezea kuwa mahusiano baina ya wananchi na masheha yamekuwa si mazuri, hivyo kuwepo umuhimu wa kutafuta suluhu ili jamii ikae kwa amani.

UMATI imeiomba Serikali ya Zanzibar kutekeleza Sheria iiyorekebishwa ya Serikali za Mitaa na Utawala wa Mikoa ya Mwaka 2014, ambayo licha ya mambo mengine yaliyomo katika sheria hiyo, inaagiza juu ya uwepo wa ofisi za masheha visiwani humo. Sheria hiyo inatambua nafasi ya masheha, tena inaitaka serikali kuwapatia ofisi na kuwalipa wasaidizi wao.

"Baada ya kutambua mianya iliyopo kwenye sheria hizi, na kuona uhusiano tete baina ya wananchi na masheha, tulitambua haja ya ushiriki wa jamii katika kuondoa uadui uliopo. Napenda kuitumia fursa hii kuishukuru FCS kwa kuufadhili mradi huu," alisema Ali Suleiman ambaye ni mfanyakazi wa UMATI.

Suleiman aliongeza kuwa; "baada ya kuanza utekelezaji wa mradi, tulitambua kuwa wananchi wengi hawakujua sheria zinazohusu ofisi za masheha za Zanzibar, huku watu wengine wakiwa hawayajui mamlaka ya masheha. Tuligundua pia kuwa masheha wengi walikuwa na uelewa mdogo wa sheria zinazowaongoza kutekeleza majukumu yao."

Sheha wa Mkokotoni, Ame Haji Ame, ambaye ni mnufaika wa mradi huu anasema ruzuku iliyotolewa na FCS kwa UMATI imechochea maelewano baina ya wananchi na viongozi wa shehia. Hata hivyo anaongezea kuwa, miradi ya uhamasishaji na uelewa iliyotekelezwa na UMATI haitoshi kumaliza tatizo hilo licha ya kukubali kuwa, UMATI imefanya kazi njema ya kuwafundisha baadhi ya sheria za uhamiaji.

"Watanzania wengi tayari wanafahamu kwamba wanayo haki ya kuishi popote pale. Wanajua kwamba wanayo haki ya kuondoka toka sehemu moja na kwenda nyingine bila kuwafahamisha viongozi.Hivi sasa, tunawashauri kutafuta barua za ufahamisho pindi wanapotaka kwenda sehemu nyingine," anasema.

Sheha huyo anaeleza kwamba, masheha wanaandika barua za utambulisho kwa watu wanaohama. "Hii inawasidia kuhudumiwa na viongozi mahalia pindi wanapotulia kwenye makazi mapya," anaeleza.

Sheha wa Pangawi, Abdallah Juma Mtumwene wa Wilaya B Magharibi, anasema kwamba mradi wa UMATI umeleta mabadiliko makubwa. Anaeleza kuwa amebadili mtazamo wake kuhusu majukumu ya wawakilishi wa shehia.

"Huko nyuma, watu wengi walitukwepa. Baada ya kupata mafunzo, wanatambua kwamba Sheha naye ni binadamu kwa hiyo anaweza kufanya makosa kama watu wengine. Kitu tunachokihitaji hivi sasa ni tafsiri ya baadhi ya sehemu za Sheria ya Mwaka 2014, ambazo zinaainisha majukumu ya masheha wa Zanzibar," anasema.

Hadija Makame, mkazi wa Mkokotoni, anasema kwamba ni vigumu kwa watu wa kawaida kuzielewa sheria zilizoandikwa kwa kiingereza. Anasema kwamba baada ya kuhudhuria mafunzo ya siku tatu yaliyoendeshwa na UMATI, amevielewa vipengele vya sheria vinavyohusiana na kazi ya masheha.

"Sikufahamu kwamba shurti tutekeleze sheria wakati wote, hata pale tunapofanya shughuli za kila siku.Sikujua kwamba ofisi ya sheha imeanzishwa kisheria. Hivi sasa natambua kuwa ni ya kisheria, kwamba zipo sheria na miongozo inayotawala utendaji wao, anasema Nassor Khamis Nassor, mkazi wa Shehia ya Magogoni iliyopo Wilaya B, Unguja.

"Huko nyuma, watu wengi walitukwepa. Baada ya kupata mafunzo, wanatambua kwamba Sheha naye ni binadamu kwa hiyo anaweza kufanya makosa kama watu wengine. Kitu tunachokihitaji hivi sasa ni tafsiri ya baadhi ya sehemu za Sheria ya Mwaka 2014, ambazo zinaainisha majukumu ya masheha wa Zanzibar," anasema.

MHNT yahamasisha

Kutoka Uk. 6

"Tayari tumeshaona mabadiliko ya mitazamo yao. Hivi sasa wana shauku ya kuzungumza kwa uwazi. Jukumu letu ni kuwafanya wawe makini na kuwasaidia waboreshe namna yao ya kufikiri pamoja na kujishughulisha na shughuli za kila siku. Tumelitembelea eneo zima la mradi. Kila siku, tunapata taarifa kuhusu matokeo ya mradi wetu," anasema.

"Hivi sasa, vijana wanaainisha aina mbalimbali za miradi wanayotaka kufanya, miradi ambayo inahusiana na hali ya maisha yao ya kila siku. Jukumu letu la msingi ni kuwawezesha kufuatilia utendaji wao wenyewe. Hata hivyo, tunayo shauku ya kupata matokeo ya kuridhisha." anafafanua.

Aliongeza kuwa: "tunatarajia kuona mabadiliko ya mitazamo ya vijana kwa kuwawezesha kuzungumza waziwazi mawazo yao. Tunapanga kuonyesha matokeo mazuri mwishoni mwa mradi."

Jonathan Mwaipopo ni mmojawapo wa wanufaika wa mradi. Anasema wazi kwamba kabla hajajiunga na majukwaa ya vijana ya MHNT, alikuwa hajui lolote kuhusu Sera ya Taifa ya Vijana.

"Sikujua kwamba Tanzania ina sera ya vijana. Ilikuwa vigumu kwangu kufahamu haki zangu. Nalishukuru shirika hili kwa kutusaidia tutambue sisi ni nani na kwa kutusaidia kujua haki zetu," anasema.

"Urahisi" wa maisha mpakani na Kenya

Kitobo, kijiji kilichopo kwenye kituo cha mpakani cha Holili, ambacho kinatenganisha maeneo ya Tanzania na Kenya, ni kitovu cha pilikapilika za wakazi wa nchi hizi mbili. Kwa ufadhili wa Trade Mark East Africa kupitia FCS mradi ulikusudia kutathmini mahusiano ya kibiashara miongoni mwa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mradi huu ulifadhiliwa na Trade Mark East Africa na kupitia shirika la Foundation for Civil Society (FCS).

Lengo la mradi ni kuongeza uelewa wa wanawake na vijana kuhusu fursa za kibiashara na masoko kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Anorld Onyango anaonekana akiendesha baiskeli na kuvuka mpaka akitokea Kenya na kuingia upande wa Tanzania, huku akiwa amebeba mfuko wa plastiki, bila shaka kipo anachokitafuta.

Onyango alieleza kwamba huko kwenye soko la Himo hununua mahindi na kuyasaga kupata unga, kabla hajavuka tena mpaka na kurejea upande wa Kenya akiwa na chakula cha kulisha familia yake.

Ninapomaliza mazungumzo yangu na Onyango, ninawaona akina mama wawili wakielekea upande wa Tanzania na kuvuka mpaka hadi Tanzania. Wamebeba mikungu ya ndizi vichwani mwao. Baada ya kuwahoji, wananiarifu kuwa wanapeleka ndizi kwenye mnada wa Himo ili waziuze.

Mmoja wao aliyejitambulisha kama Hilda, anasema anaishi upande wa Kenya, na siku zote amekuwa akipeleka vyakula kwenye soko la Himo ili kuviuza.

Upande wa Tanzania, nawaona vijana wawili wakivuka mpaka kuingia Kenya huku wakiwa wamebeba madumu matupu. Baada ya kuwadadisi, wananiambia kwamba wanakwenda upande wa Kenya ili kununua mafuta ya taa na majani ya chai.

Taswira hii inaonyesha jinsi watu waishio sehemu za mpakani wanavyorahisisha maisha kwa kuukataa mpangilio mpya wa dunia, ambao unaiona mipaka kama alama dhahiri zinazowatenganisha watu daima, labda tu pale hati za usafiri zinakapotumika, au iwapo upo utaratibu maalum wa kuwawezesha watu watembee kwa uhuru.

Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, uvukaji huria wa mipaka waweza kutokana na historia ya huko nyuma kuhusiana na Mkataba wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inayojumuisha nchi za Kenya, Uganda na Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, ambao uliruhusu uhuru wa watu kutoka sehemu moja hadi nyingine ndani ya Jumuiya, kama mojawapo wa vipengele muhimu vya ushirikiano.

Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zilipitisha utaratibu wa uvukaji huria wa mipaka kwa watu, nguvukazi na huduma, pamoja na haki ya kuanzisha makazi ya wananchi kwenye eneo la Afrika Mashariki chini ya Kifungu 104 cha Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Uzinduzi rasmi wa hati za kusafiria za Afrika ya Mashariki ulifuata mnamo mwaka 1999. Hati hizo zilianza kutumika, nazo zikawawezesha wananchi wa Afrika Mashariki kusafiri kwa uhuru ndani ya eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kipindi cha miezi sita.

Upande wa Kaskazini ni makazi ya miji midogo ya Holili na Taveta. Mabasi ya shule yanaonekana yakibeba wanafunzi kutoka Tanzania kuingia Kenya, pia kutoka Kenya kuingia Tanzania. Mwelekeo huu unadhihirisha kwamba watu wa eneo hili wameamua kuyafanya maisha yawe rahisi.

David Wanyoke, mwendesha pikipiki iliyosajiliwa Kenya, anakiri kwamba anao uhuru wa

Inaendelea Uk. . 12

FCS yarekebisha Dhana yake ya Mabadiliko

Foundation for Civil Society (FCS) imeipitia upya na kuiboresha Dhana yake ya Mabadiliko (Theory of Change) inayohusisha pia maeneo ya upatikanaji Matokeo, Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo. Dhana hii ya Mabadiliko itaiwezesha FCS na wafadhili wake wakuu kuandaa ripoti za nusumuhula, za kila mwaka na kila baada ya miaka mitano; lengo likiwa kutathmini namna miradi inayotekelezwa na FCS imefikia matokeo yanayotarajiwa. Kwa kufanya hivyo, dhana hii itasaidia kuonesha maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa na yale yaliyoonesha mafanikio.

Dhana hii itaiwezesha FCS kutumia mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo kama zana ya usimamizi na kufanya maamuzi na pia kuunganisha mfumo huo na utaratibu uliopo wa usimamizi wa ruzuku.

Ili kuupa nguvu mchakato mzima wa kuiangalia upya dhana hii, INTRAC, ambayo ni kampuni ya ushauri wa kitaalamu, ilipewa jukumu la kutathmini mfumo wa FCS wa Ufuatiliaji, Tathmini, na Mafunzo pamoja na Dhana ya Mabadiliko.

Mchakato huu ulianza Desemba 2016, ambapo wataalam washauri walifanya mikutano kwa njia ya simu na watu wa FCS na wale wa DFID jinsi mchakato unavyoweza kuwa halisi kwa kujadili hadidu rejea, maandishi ya awali na mapitio ya machapisho.

Washirika wote wa Maendeleo walishiriki kwenye warsha moja au zaidi ambapo mchakato wa Dhana ya Mabadiliko ulijadiliwa. Warsha hizo zilifanyika kati ya Januari 23 na 27 kwenye Hoteli ya Bahari Beach, Dar es Salaam.

Warsha kuhusu Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo ilifanyika kati ya Februari 13 na Februari 17, 2017 kwenye Ukumbi wa mikutano wa FCS na kuwashirikisha wafanyakazi wa FCS na Mtaalamu Mshauri.

Washiriki waliiangalia kwa kina Dhana ya Mabadiliko iliyoandaliwa, nao wakaanza kutengeneza Mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo kwa ajili ya mpango wa Utawala Bora na Kujenga Uwezo.

MAREKEBISHO YA DHANA YA MABADILIKO YA FCS

Wajumbe wa Bodi ya FCS, Washirika wa Maendeleo, Timu ya Uongozi na Washiriki kutoka asasi mbalimbali wakihudhuria warsha katika hoteli ya Ledger Plaza Bahari Beach, mwanzoni mwa mwaka huu. Warsha hiyo ilirekebisha Dhana ya Mabadiliko ya FCS na kubainisha njia za kuifikia.

Summary Representation of FCS Theory of Change

What FCS does	So that our grantee CSOs	So that we achieve these changes in the areas where we work by 2020		.... and contribute to these longer term changes	Our vision of success
We leverage resources & manage development grants.	Set up sound policies and practices and demonstrate fair, transparent and accountable leadership	**CSOs are strong, coordinated and able to serve their constituencies effectively and efficiently**	LGAs deliver improved quality services	Government is more transparent, democratic, accountable & responsive to its citizens' needs and aspirations.	**Empowered and responsible Tanzanians realize social and economic justice and improved quality of life**
We strengthen the capacity of key development actors.	Ensure good working environments and retain staff		Decision-making and democratic processes better reflect citizens' rights groups, PWDs and minority and women	Better policies laws and regulations empower communities and guide participation, compliance and accountability.	
We cartelize strategic linkages and partnerships.	Effectively manage FCS funded thematic projects and programs		Communities have strong capacities and institutions for dialogue and conflict management	Civil society is more vibrant, better governed, more sustainable, and effectively delivering on its mandates.	
We facilitate research, analysis, creation & sharing of knowledge to shape policy and learning.	Set up networks and engage in joint advocacy		Small holder farmers have access to extension services and improved security of tenure	Citizens, especially excluded groups, have increased access to assets, resources, opportunities and entitlements	
We invest in our capacity to enable better deliver our ambitions.	Invest in joint learning and sharing across the sector		Youth and women entrepreneurs have secured greater access to markets, livelihood assets and resources	More targeted citizens are empowered, responsible, actively engage in critical governance processes and holds government to account.	

Principles and Assumptions:
Well-resourced and capable civil society can play a critical role contributing to good governance. CSOs also have a shared responsibility for developing people's capabilities and improving power relations, in ways that actively engage the people themselves. Processes towards improving governance are however complex and unpredictable hence call for regular context analysis to inform action. Achieving sustained change also requires collaboration amongst key actors.

MAHOJIANO

Edna Chilimo: Mtaalamu wa kujenga uwezo kwa Azaki

Ulianza lini kufanya kazi FCS?
Nilianza kufanya kazi mnamo Juni 2015 kama Meneja wa Kujenga Uwezo. Kabla ya hapo, nilikuwa nimeajiriwa kwenye Kituo cha EASUN kwenye Programu ya Mafunzo iliyojulikana kama BOCAR (Kujenga Uwezo wa Kitaasisi ili Kuleta matokeo) kama Afisa Mradi Mwandamizi kwa miaka minne.

Ni yapi majukumu yako hapo FCS?
Jukumu langu kuu ni kuonyesha uongozi wa kimkakati kwa ajili ya kujenga uwezo wa FCS. Shughuli hiyo inajumuisha kubuni njia na mbinu bora zitakazoiwezesha FCS kubakia kama kiongozi wa sekta ya asasi za kiraia nchini Tanzania. Natakiwa kutoa mwongozo wa kitaalamu kuhusiana na ujenzi wa uwezo wa taasisi za kiraia na kuhakikisha utoaji wa maelekezo ya kitaalamu kuhusiana na kujenga uwezo wa taasisi, pamoja na kuhakikisha kuwa wataalamu wa nje wanatoa huduma bora. Vilevile ninalo jukumu la kusimamia mtandao wa ushirikiano kwenye sekta ya asasi za kiraia pamoja na kujenga mahusiano baina ya sekta ya asasi za kiraia na waleta maendeleo wengine.

Unayatekeleza vipi majukumu hayo?
Daima najifunza kutoka kwenye uzoefu wangu na kwa wengine. Nachota ujuzi wa wataalamu wa maendeleo ya mashirika maarufu ulimwenguni kama Ricky James wa INTRAC, ambaye namfuatilia kwenye mitandao ya kijamii. Najifunza kutokana na matamko yao, vitabu vyao na maandishi mbalimbali. Najitahidi kuyaelewa maandishi mapya yanayouhusu ujenzi wa uwezo wa taasisi, ili niendane na mienendo ya kujenga uwezo. Nalipia uanachama wa majukwaa kadhaa ya elimu-mtandao na kuhudhuria kozi mbalimbali za kimtandao, yaani semina za kimtandao ambapo wanafunzi wanamwona mwalimu na kuuliza maswali. Ninaye mshauri ambaye naweza kuwasiliana naye kwa ushauri wa kitaalamu au mawaidha. Kwa kufanya hivyo, naimarisha utendaji wangu na ule wa idara. Muhimu zaidi, ni kwamba imani yangu kuhusu kufanya kazi kama timu pia kama mtandao inanisaidia kuhuisha na kuyamudu majukumu yangu.

Ni changamoto zipi zinazozikabili asasi za kiraia nchini Tanzania katika kujenga uwezo?
Asasi za kiraia nchini Tanzania zinakabiliwa na changamoto nyingi. Baadhi ya changamoto hizi ni za kawaida nazo zimekuwapo kwa muda mrefu. Kwenye mstari wa mbele wa changamoto hizi, kuna ukosefu wa mtazamo wa kimkakati kutokana na uwepo wa ujuzi haba wa usimamizi wa mikakati. Kwa viongozi, hili linasababisha uwezo mdogo wa kupata maono yenye kuleta mafanikio kwa siku zijazo. Viongozi kama hawa wa asasi za kiraia hushindwa kujipambanua dhidi ya maelezo ya siku kwa siku. Wanashindwa pia kuliongoza shirika dhidi ya misukumo ya mabadiliko. Pale ambapo viongozi na wafanyakazi wana uwezo wa kimkakati, taasisi itajenga na kuainisha mwelekeo wake.
Hali hii itawalazimisha kuchagua mwenendo ambao shirika litachukua ili kukabiliana na hali iliyopo ili iendane na mazingira pia na matokeo yake kwa asasi kwa namna mbalimbali.
Changamoto nyingine ni kwa hali ya asasi zisizokuwa za kiserikali kushindwa kupata michango kutoka kwa wahisani wa ndani.
Changamoto hii ni matokeo ya ukosefu wa ujuzi wa mbinu au uelewa wa uwezekano wa uwepo wa uhisani wa ndani. Pindi uhisani wa ndani unapotafutwa na kuanzishwa, unaweza kuilinda ajenda ya asasi za kiraia, ili kumudu kutekeleza agenda za ndani kwa rasilimali za ndani.
Utawala bora pia ni changamoto ambayo imekuwa ikizikabili asasi za kiraia kwa kipindi fulani, licha ya juhudi zilizokwisha fanywa. Iwapo uzoefu ni fundisho, inatosha kusema kwamba ugonjwa wa waanzilishi (ambapo wanakuwa na madaraka na ushawishi usiokuwa na kikomo) ndiyo sababu kubwa ya ukosefu wa utawala bora kwenye asasi za kiraia.
Waanzilishi wengi wanaonekana kuwa na madaraka yanayozidi yale ya Bodi za Wakurugenzi. Tukitamka kwa uhalisi, ufumbuzi wa tatizo la utawala bora unahitaji kabisa kubadilika kwa mioyo ya waanzilishi wa asasi zisizokuwa za kiserikali.
Changamoto nyingine yenye uwezo wa kuleta matatizo ni kushindwa kwa asasi zisizokuwa za kiserikali kutoa taarifa ya kazi njema ambayo wamefanya. Kwenye suala hili, kumekuwa na mang'amuzi yanayokinzana.
Baadhi ya asasi zina uwezo mdogo wa kutekeleza miradi, lakini zina uwezo mkubwa wa kuandika na kutoa taarifa za matokeo. Kwa upande mwingine, asasi nyingine zina uwezo mkubwa wa utekelezaji wa miradi, lakini ni dhaifu katika kueleza mafanikio. Hali hii inailazimu FCS na wafadhili wa asasi zisizokuwa za kiserikali kuchangia zaidi ili kuimarisha uwezo wa asasi za kiraia kulingana na mahitaji. Hiki ndicho ambacho FCS inafanya hivi sasa.

FCS imeipitia upya Dhana yake ya Mabadiliko. Je, Dhana hii itawezaje kuhuisha kazi ya asasi zinazopata ruzuku kutoka FCS?
Dhana yetu ya mabadiliko ya asasi za kiraia yafaa iangaliwe kwa mtazamo wa mfumo ambapo masuala, matukio na nguvu zilizomo ndani ya asasi za kiraia hazitengani bali zinahusiana, ambapo sehemu moja ya asasi ina athari kwenye sehemu iliyosalia. Kwa hiyo, tumebuni mwenendo wetu wa kujenga uwezo katika utatu, yaani, uwezo unaohusiana na uimarishaji wa taasisi, uwezo wa kufanya ambao unahusiana na uimarishaji wa utendaji wa mradi pamoja na uwezo wa kuandaa wasifu wa sekta na uendelevu. Kinyume cha desturi za zamani, mkakati wa FCS utahusisha tathmini iliyofanywa kwa uangalifu kuhusu uwezo wa washirika wake na uwezeshaji wa ujenzi wa uwezo uliopangwa na wenye msukumo wa kuzaa matokeo katika maeneo yaliyoainishwa. FCS itatumia asilimia 10 tu ya rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya uimarishaji wa taasisi (uwezo wa kuwa), asilimia 70 kwa ajili ya uwezo wa kutenda, yaani kuimarisha uwezo wa utekelezaji wa miradi, na asiimia 20 kwa ajili ya uwezo wa mahusiano.

Asasi zapambana na unyanyapaa wa Watu Wenye Ulemavu Biharamulo

Padre Honoratus Ndaulla (kulia), Mratibu wa Mradi wa Wadhamini Waliosajiliwa wa Jimbo Katoliki la Rulenge-Ngara kwenye picha ya kikundi na baadhi ya wanufaika wa mradi unaofadhiliwa na FCS unaohusu haki na majukumu ya Watu Wenye Ulemavu.

'Ulemavu si kutoweza.' Huu ni msemo unaowapa moyo Watu Wenye Ulemavu watambue kwamba hali yao haiwazuii kufanikisha ndoto zao.

Usemi huo pia unalenga kubadili mtazamo wa watu ambao si walemavu, ili waweze kuwaona kuwa walemavu ni wanadamu wenzao ambao wana uwezo wa kufikia malengo yao ya kimaisha kama watu wengine.

Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa Ban Ki-Moon, kwenye mkutano uliofanyika mwaka 2013, alisema: "Ulemavu ni sehemu ya hali ya binadamu. Kwenye kipindi fulani cha maisha, karibu kila mtu anaweza kuwa mlemavu wa muda au siku zote za maisha yake."

Kulingana na kauli hiyo ya Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa, mnamo mwaka 2013, kulikuwa na zaidi ya watu bilioni moja wenye ulemavu duniani kote, hii ikiwa ni asilimia 15 ya idadi ya watu duniani ya wakati huo.

Sensa ya Taifa ya Mwaka 2012 ilionyesha kwamba Tanzania ilikuwa na idadi ya watu 44,928,923, ambapo watu 43,625,354 walikuwa Tanzania Bara na 1,303,569 walikuwa Zanzibar. Wanaume walikuwa 21,869,990 na wanawake walikuwa 23,058,933.

Licha ya kwamba takwimu kuhusu Watu Wenye Ulemavu ni muhimu, haki na wajibu wa kundi hili ni za muhimu zaidi kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha unyanyapaa kwenye jumuiya mbalimbali.

Katika Wilaya ya Biharamulo, Asasi isiyokuwa ya kiserikali ijulikanayo kama Registered Trustee of Roman Catholic Diocese of Rulenge-Ngara, ambayo inafadhiliwa na FCS, inawahamasisha Watu Wenye Ulemavu, wafanya maamuzi na viongozi kufahamu haki na wajibu wa Watu Wenye Ulemavu.

Asasi hiyo imeamua kutekeleza jukumu hilo baada ya kutambua kuwa, Watu Wenye Ulemavu kwenye Wilaya ya Biharamulo wanatambuliwa kwa ulemavu wao badala ya majina yao halisi.

Kazi hiyo ilitanguliwa na utafiti wa awali, uliolenga kuwaorodhesha watu wote wenye ulemavu katika wilaya nzima ya Biharamulo, kabla ya kukikusanya kikundi cha wadau ambao wangehudhuria semina za uhamasishaji. Wilaya hiyo ina kata 17 zenye vijiji 79. Mpaka sasa, kampeni za uhamasishaji zimefanyika kwenye kata tisa kwenye robo ya kwanza ya kipindi cha utekelezaji.

Padre Honoratus Ndaulla, Mratibu wa Miradi ya shirika hilo, anasema kwamba baadhi ya wanasiasa na viongozi wa serikali za mitaa wamehudhuria semina za uhamasishaji. Walioshiriki ni pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, madiwani, Mkurugenzi na watendaji wa Wilaya.

Padre Ndaulla anasema kwamba, ilikuwa ni lazima kuwahusisha wanasiasa na viongozi wa serikali kwa kuwa wao ndiyo wenye jukumu la kuwahudumia Watu Wenye Ulemavu kwenye maeneo yao. Alisema kwamba wakati wa utafiti, aligundua kuwapo kwa hali ya ubaguzi na kutojali ya jamii kuhusiana na Watu Wenye Ulemavu, ambayo iliifanya asasi itafute njia ya kuubadilisha mwelekeo huo.

Akitoa mfano, Padre Ndaulla alisema kwamba Watu Wenye Ulemavu wilayani Biharamulo hawakuzingatiwa na serikali kuu na za mitaa wakati wa uchoraji wa ramani ya majengo ya umma. "Nenda mahakamani, hospitalini, kwenye shule, vituo vya polisi na majengo mengine ya serikali," alisema.

Aliongeza: "Maofisa wa serikali wanalo jukumu la kuhakikisha kwamba Watu Wenye Ulemavu wanahudumiwa kwa haki au kwa namna maalum katika utoaji wa huduma. Hilo ndilo tunalowaambia tunapokutana nao kwenye warsha tunazoziandaa."

Shuhuda za Watu Wenye Ulemavu

Baadhi ya Watu Wenye Ulemavu walitoa ushuhuda kutokana na msaada waliopata kutoka kwenye asasi hiyo. Paul Makene, mtu mwenye ulemavu, alikumbuka kuhusu faida za mradi na kusema kwamba, kwa miaka mingi Watu Wenye Ulemavu wa Biharamulo walipata matatizo ambayo yalihitaji kushughulikiwa na viongozi wa wilaya. Hata hivyo, hawakufanikiwa kupata jukwaa la kuzungumzia kero zao.

Alisema kwamba kwa Watu Wenye Ulemavu, fursa ya kukutana ana kwa ana na Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya, Wawakilishi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Madiwani, iliwapatia nafasi ya kueleza mahitaji yao. Akitoa mfano, Makene alisema: "Baadhi ya majengo ya serikali wilayani Biharamulo hayana mazingira rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu kama mimi. Leo hii tuna furaha kwa sababu serikali inafanya juhudi za kuirekebisha hali hiyo."

Makene, ambaye aliwahi kugombea uongozi wa serikali ya mtaa, alisema kwamba, wapinzani wake waliutumia ulemavu wake kumshambulia ili kujenga taswira kwa wapiga kura kwamba ulemavu ni ukosefu wa uwezo.

Kwa maelezo ya Makene, ilikuwa kawaida kwa wazazi wenye watoto walemavu kuwaficha ili wasionekane hadharani. "Mradi wetu unafanya shughuli ambazo zitaibadilisha mila hii," alisema.

"Viongozi wa semina walipotualika kuhudhuria semina, nilikutana na watu wenye aina mbalimbali za ulemavu ambao sikuwahi kuuona. Hii ilikuwa ishara kwamba walikuwapo watu wengi waliokuwa na hali kama hiyo, ambao walifichwa na wazazi na walezi wao ili wasionekane hadharani,"alisema.

Mviwata yapunguza migogoro ya ardhi Songea

Washiriki wakifuatilia mafunzo kuhusu upatikanaji wa haki za ardhi iliyoandaliwa na MVIWATA

Kwenye nchi ambayo karibu asilimia 80 ya wananchi wanategemea kilimo kama njia ya kipato, ujuzi wa sera na sheria unahitajika kupewa kipaumbele kwenye mipango ya taifa.

Ingawa serikali inalo jukumu la pekee la kuhakikisha kwamba wananchi wanaelimishwa kuhusu masuala ya ardhi na haja ya kuwa na ubadilishanaji wa umiliki wa ardhi kwa njia ya amani, wadau wengine, ikiwemo FCS, wanalo jukumu lao vilevile. Asasi za kiraia nazo zina mchango wake katika kupunguza migogoro ya ardhi kwa kutoa elimu na kuongeza uelewa wa masuala ya sera na sheria zinazohusu umiliki wa ardhi.

Mkoani Ruvuma, Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), kutokana na ruzuku inayotolewa na FCS, imefanikiwa kupunguza migogoro ya ardhi baina ya familia au jamii mbalimbali. Mradi wa MVIWATA, unaojulikana kama Acha Uporaji wa Ardhi, Linda Haki Zako umetekelezwa kwenye vijiji 13 kwenye kata nne za Wilaya ya Songea Vijijini tangu Oktoba 2016.

Migogoro isiyoisha, ambayo mara nyingi huwa na mwisho mbaya kwa washiriki migogoro hii ya ardhi na ambayo mara nyingi hutokana na kutokuelewa sheria mbalimbali zinazosimamia umiliki wa ardhi, hasa sheria za umiliki wa ardhi na vipindi vya umiliki, ni baadhi ya mambo yaliyoifanya asasi hiyo kutafuta ruzuku ili kutekeleza mradi kwenye kata za Mpitimbi, Maguguta, Muhulutwe na MpandaNgido.

Graciana Ntango, mmoja wa wajitoleaji kwenye Kijiji cha Mpandangido, anao ushahidi wa kudhihirisha kuwa, mradi huo ulipokuwa na miezi mitatu tu tayari ulidhihirisha mafanikio makubwa. Alikuwa mmojawapo wa wakufunzi walioelimishwa kuhusu masuala ya ardhi, ikiwemo Sheria ya Ardhi No. 4 ya Mwaka 1999 pamoja na haki za watu binafsi na vijiji kuhusiana na umiliki wa ardhi.

Jukumu la Wakufunzi, kulingana na kauli ya Meneja Mawasiliano Denis Mpagazi, lilikuwa katika maeneo matatu: kuwaelewesha wanavijiji kuhusu Sheria ya Ardhi, kuwa kiungo baina ya mabaraza ya ardhi na serikali za mitaa katika Wilaya ya Songea Vijijini, na pia kuiarifu MVIWATA kuhusu kesi za ardhi zinazoendelea kwenye vijiji vyao.

"Urahisi" wa maisha...

Kutoka Uk. 8

w kuchagua Holili upande wa Tanzania au Taveta upande wa Kenya kama kituo cha kubeba abiria kila siku.

"Uzuri ni kwamba naweza kufanya shughuli zangu upande wowote wa mpaka bila kukabiliwa na tatizo lolote. Ndiyo maana unaniona hapa hivi sasa," Wanyoike anasema.

Matumizi ya sarafu mbili

Tuliwaona abiria wa bodaboda wakivuka aidha upande mmoja wa mpaka au mwingine. Wanao uhuru wa kufanya malipo aidha kwa fedha za Kenya au Tanzania.

"Tunatumia fedha za aina mbili iwe Holili au Taveta. Utaratibu huu hauleti matatizo yoyote, labda tu pale mtu anapotaka kwenda ndani zaidi ya Kenya au Tanzania," Onyango anasema.

Utafanya nini iwapo nyumba ya jirani yako itashika moto?

Rais wa zamani wa Marekani, Franklin Delano Roosevelt, aliwahi kutamka kwamba iwapo nyumba ya jirani yako itaungua, huna haja ya kubishana kuhusu bei ya mpira wako wa maji. Kuishi mpakani kuna faida nyakati nyingine na hasara nyakati fulani fulani, kwani iwapo tatizo litatokea upande wowote ule wa mpaka, wakazi wa pande zote mbili huenda wataathiriwa.

Robert Ngui, raia wa Kenya aishiye mita chache kutoka mpaka wa Tanzania kwenye Kijiji cha Kitobo, analalamika kuhusu kupanda kwa bei ya chakula nchini Tanzania. Anadai kwamba anaathirika sana na hali hiyo.

"Ujue kwamba sisi Wakenya tunategemea upatikanaji wa chakula kutoka Tanzania. Kwa bahati mbaya, bei za vyakula zimepanda sana. Tunamwomba Rais Magufuli atafute njia za kulishughulikia suala hili kwa kuwa hivi sasa, maisha yanakuwa magumu," raia huyu wa Kenya anatamka.

Ngui alisema kwamba siku za nyuma, gunia la mahindi lenye uzito wa kilo 100 lilikuwa likiuzwa kwa shilingi za Tanzania 42,000. Lakini hivi karibuni, bei imefikia shilingi za Tanzania 120,000.

Vipi kuhusu huduma nyingine?

Ngui anasema kwamba watu wanaoishi pande zote za mpaka wanatumia huduma zilezile za matibabu, elimu na maji. "Wazazi wanaweza kuwapeleka watoto wao kwenye shule zilizopo upande wa Kenya, ambapo wazazi wa Kenya wanaweza kuwapeleka watoto wao kupata masomo upande wa Tanzania.

Kulingana na maelezo ya Ngui, wakazi wa Kenya waliopo mpakani hupata matibabu kwenye zahanati za Tanzania kutokana na ukaribu na urahisi wa kufika. Kwa upande mwingine, wanafunzi wa Tanzania wanasoma upande wa Kenya, hasa Taveta, kutokana na ubora wa elimu inayotolewa.

Cornel Mushi, mkazi wa Holili, anasema kwamba wengi wa Watanzania wanapendelea kuwapeleka watoto wao kusoma kwenye shule zilizopo upande wa Kenya kwa ajili ya kupata ufanisi wa matumizi ya lugha ya Kiingereza.

"Kila mzazi anapenda kuona mtoto wake akiongea Kiingereza sanifu. Wazazi wa Tanzania wanaitumia fursa hii kuwapeleka watoto wao kwenye shule za Kenya. Iwapo utakuwa hapa hadi saa za jioni, utayaona magari yaliyosajiliwa Kenya yakiwarudisha watoto kutoka upande wa Kenya," Mushi anasema.

Marufuku ya kuvusha vyakula mpakani

Afisa doria ya mpakani mwenye jukumu la kudhibiti upitaji katika njia zisizo halali maarufu kama njia za panya katika Kijiji cha Kitobo, anayejulikana kwa jina la Sudi, anasema kwamba hairuhusiwi kabisa mizigo ya chakula kuvuka mpaka. "Sisi tunaruhusu uvushaji wa vyakula kwa lengo la matumizi binafsi au ya familia tu," anasema.

Mkuu wa Mkoa aisifu asasi ya kiraia kwa kupiga vita mimba za utotoni

Mhe. Godfrey Zambi, Mkuu wa Mkoa Lindi

Hapa yupo msichana, waweza kumwita Bi. X. Anaonekana ana umri usiotimia miaka 18. Ni mjamzito. Yaelekea kuwa mimba za utotoni ni jambo la kawaida hapa Lindi.

Nasogea karibu na kumhoji kuhusu ujauzito wake. Ananitazama kwa mashaka. Inaelekea kuwa hakutegemea kupata swali lolote kutoka kwangu. Baada ya muda, ananijibu. Bi. X ana umri wa miaka 16. Ni mkazi wa Kilwa Masoko Mkoani Lindi.

Aliacha shule akiwa na umri wa miaka 11 na kuolewa mwaka uleule. Ndoa yake ilikaa kwa muda mfupi. Mumewe aliamua kutoroka. Upo msemo wa Kiswahili usemao kwamba "jambo usilolijua ni sawa na usiku wa giza." Kwa kweli, hii si mimba yake ya kwanza". Anaye mtoto mwenye umri wa miaka miwili huko nyumbani.

Wapo akina mama wengi wenye umri mdogo Kusini mwa Tanzania. Inasemekana kwamba mazingira, utamaduni na mila ni baadhi ya mambo yanayosababisha ndoa na mimba za utotoni. Uongozi dhaifu wa familia na kiu ya utajiri huwafanya wasichana wengi kuondoka nyumbani na kuolewa. Baadhi yao wana umri chini ya miaka 18.

Godfrey Zambi, Mkuu wa Mkoa Lindi, anapoulizwa kutoa maoni yake, anasema kuwa mimba za utotoni na ndoa za utotoni zinasababishwa na malezi duni toka kwa wazazi na suala zima la umaskini. "Familia zinapendelea kuwalazimisha wasichana wadogo waolewe kwa ajili ya kupokea mahari," anasema.

Mila za kufundwa zijulikanazo kama jando na unyago pia zinasababisha ndoa za awali na mimba za utotoni. "Sherehe za jando na unyago kwa kawaida ni kwa ajili ya kuwafunda vijana. Wakati wa sherehe hizi, vijana wanafundishwa kudhibiti vishawishi vya ngono," Zambi anasema. Anaongeza kuwa, kwenye wilaya za Liwale, Kilwa, Nachingwea na Lindi vijijini, shughuli kama hizo ni za kawaida.

Upo ukweli unaodhihirishwa kisayansi kwamba mimba za utotoni, hasa kwa wasichana walio na umri chini ya miaka 18, zaweza kusababisha vifo kwa wazazi wenye umri mdogo. Wasichana walio na umri chini ya miaka 18 wanafikiriwa kuwa hawajakomaa kwa mambo ya uzazi.

Rekodi zilizopo zinaonyesha kuwa kulikuwa na mimba 32 za wasichana walio chini ya miaka 18 mkoani Lindi mwaka 2016. "Tunashirikiana na asasi za kiraia zilizopo Lindi kuielewesha jamii kuhusu matatizo yanayosababisha mimba za utotoni na ndoa za utotoni," anasema Mkuu wa Mkoa Lindi.

Kwa upande wake, Kituo kiitwacho Lindi Women Paralegal Aid Centre, huendesha semina mbalimbali za wanawake na watoto. Mkurugenzi wa kituo Cosma Bulu, anasema pia kuwa mimba za utotoni zinasababishwa na mila potofu.

CHAVITA: Huduma za afya kwa watu wenye ulemavu wa kusikia

Watu wenye ulemavu wa Usikivu wamepata njia mpya ya maisha baada ya watoa huduma za afya kuhudhuria mafunzo ya lugha ya Alama. Kozi hiyo iliendeshwa na Chama cha Walemavu wa Usikivu cha Tanzania (CHAVITA), Tawi la Tabora.

Mwenyekiti wa CHAVITA Tawi la Tabora, Ramadhan Rajab, anasema kuwa mradi wa mafunzo ya lugha ya Alama ni hatua kubwa kwa watu wenye ulemavu wa kusikia katika kupata huduma za afya. Mpaka sasa, mradi huo umehudumia vituo vya afya 53 katika Mkoa wa Tabora. Mradi huo umefadhiliwa na FCS.

"Hali imekuwa bora zaidi. Watu wenye ulemavu wa kusikia nao wanafurahi. Hapo zamani, ilikuwa vigumu kwao kuwasiliana na wafanyakazi wa afya," Rajab anasema.

Anaendelea kutamka kwamba; "walitilia mkazo suala la mafunzo ya wafanyakazi wa afya kwenye hospitali ya Mkoa na Hospitali ya Jeshi ya Milambo," alisema na kuongeza:

"Tulifanya hivyo kwa kuwa hospitali hizi mbili ni vinara wa huduma ya afya mkoani Tabora."

Dr. Joel Hoza wa Hospitali ya Mkoa ya Kitete alisema kuwa, mafunzo hayo yalikuwa na msaada mkubwa kwa kuwa wafanyakazi wa afya walikuwa hawana ujuzi unaotakiwa wa kuwahudumia wagonjwa wenye ulemavu wa Usikivu.

"Mojawapo ya matatizo ilikuwa jinsi ya kuuliza historia ya afya na ishara za ugonjwa kwa mlemavu wa usikivu. Mafunzo haya yametusaidia namna ya kuwasiliana na Watu Wenye Ulemavu.

Dkt. Joel Hoza akimhudumia mgonjwa mwenye ulemavu wa Usikivu

"Hapa Tabora, ipo Shule ya Sekondari ya Kazima, ambayo ina wanafunzi walemavu. Hawa huja kwenye hospitali yetu kwa matibabu. Siku moja, baada ya kuhudhuria mafunzo ya jinsi ya kuwasiliana na wagonjwa wenye ulemavu wa kusikia, wanafunzi watatu wa kike walikuja kwa ajili ya matibabu.

"Nilitoa ishara ya kutaka kuwasiliana nao kwa lugha ya alama. Walifurahi sana. Waliuomba utawala wa hospitali kuweka mfanyakazi mmoja ambaye angewasiliana nao kwa lugha ya Alama," alisema Dr. Hoza.

Akizungumzia ugumu wa kujifunza lugha ya alama, Margaret Kanola, mfanyakazi wa Hospitali ya Kitete, anasema ilikuwa vigumu kuelewa wanayofundishwa, kwa kuwa hawakuwa na muda wa kutosha wa mafunzo kwa vitendo.

Uswisi waadhimisha Tamasha la tano la Azaki Tanzania

Tarehe 16 Machi, 2017 Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania uliadhimisha kwa mara ya tano, Tamasha la Asasi za Kiraia (AZAKI) nchini Tanzania katika Hoteli ya Coral Beach, jijini Dar es Salaam. Tamasha hilo lilihudhuliwa na mgeni rasmi Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Mheshimiwa Frolence Mattli.

Tamasha la Asasi za Kiraia linaloandaliwa na Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania hukutanisha Azaki mbalimbali zinazopata ufadhili kutoka shirika la SDC zilizopo nchini Tanzania. Mada iliyojadiliwa katika tamasha la mwaka huu ilihusu namna Azaki zinavyojihusisha na suala la jinsia; ambapo kila asasi iliyoshiriki ilitakiwa kuelezea mafanikio yake na changamoto za kiutendaji katika suala hilo.

Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Mheshimiwa Frolence Mattli, akitoa hotuba yake ya ufunguzi katika hafla hiyo.

Balozi wa Uswisi nchini Tanzania Mheshimiwa Frolence Mattli, akiwa na Meneja wa Idara ya Maendeleo ya Biashara na Ushirikiano kutoka FCS Bi. Martha Olotu

Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation for Civil Society (FCS) Wakili Francis Kiwanga, akichangia mada katika hafla hiyo.

Sehemu ya wahudhuriaji wa hafla hiyo wakisikiliza mada kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Actions for Democracy and Local Governance (ADLG) iliyopo Mwanza Bw. Jimmy Luhende

Mwakilishi kutoka BBC nchini Tanzania akizungumza wakati wa hafla hiyo

Meneja wa Idara ya Maendeleo ya Biashara na Ushirikiano kutoka FCS Bi. Martha Olotu akitoa maelezo kwa washiriki kuhusu mafanikio na changamoto kutoka FCS katika suala la jinsia kwa mwaka 2016.

FCS yawaaga wafanyakazi wake

Foundation for Civil Society (FCS), mwezi Februari mwaka huu, iliwaaga wafanyakazi wake wanane waliomaliza muda wao wa utumishi. Wafanyakazi hao ni: Thadeo Lupembe (Kaimu Meneja wa Fedha na Operesheni), Marylin Elinawinga (Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani), Vincent Nalwendela (Mkuu wa Mawasiliano), Nestory Mhando (Ofisa Mwandamizi wa Programu-Ruzuku), Kemilembe Mpinga (Afisa Programu Msaidizi), Gladys Mkuchu (Afisa Programu, Mawasiliano), Chrispina Mwacha (Afisa Programu Msaidizi-Kujenga Uwezo) na Kasoga Kasika (Mkaguzi wa Ndani).

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Bw. Francis Kiwanga, alisema kuwa FCS inajivunia utumishi wao wa kuigwa. Alisema kwamba watumishi hao wameondoka wakiwa na uzoefu wa kutosha na sifa ya kuwa mabalozi wema wa FCS. Sherehe hiyo, iliyofanyika kwenye ofisi za FCS Jijini Dar es Salaam, zilihudhuriwa na wafanyakazi.

Bi. Gladys Mkuchu, Afisa Programu wa zamani-Mawasiliano, akipokea zawadiyake kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji, Bw. Francis Kiwanga.

Bw. Nestory Mhando, Afisa Programu Mwandamizi wa zamani-Ruzuku akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji Bw. Francis Kiwanga.

Bi. Kamilembe Mpinga (Afisa Msaidizi wa Programu wa zamani-Ruzuku) akiongea wakati wa sherehe hiyo.

Bw. Vincent Nalwendela (Mkuu wa Mawasiliano wa zamani) akiongea wakati wa sherehe hiyo.

Picha ya pamoja ya baadhi ya wafanyakazi wa FCS na wale wanaoondoka.

Ngoma maalum ya Kwaito ikichezwa nabaadhi ya wafanyakazi wa FCS waliohudhuria hafla hiyo.

ORODHA YA TAASISI ZILIZOIDHINISHWA KWA UFADHILI 2016/2017

SN	ORGANIZATION NAME	PROJECT NAME	AREA OF INTERVENTION	REGION	PAID AMOUNT-Tshs
1	ACTION FOR JUSTICE IN SOCIETY (AJISO): P.O.Box 272 Kilimanjaro; 0767/0784 816 700, Virginia Calist Silayo- Mkurugenzi Mtendaji	Tuwalinde	Citizen's Participation, voice and inclusion	KILIMANJARO	27,142,000
2	ANTI-FEMALE GENITAL MUTILATION NETWORK(AFNET): P.O.Box 1763 Dodoma; 0754/0784/0622 294 901, Mrs Sarah Daimon Mwaga-Executive Director	Stronger voices against gender based violence	Citizen's Participation, voice and inclusion	DODOMA	38,474,110
3	ARUSHA MUNICIPAL COMMUNITY FOUNDATION - P.O.BOX 2076 ARUSHA 713245861-ERNEST S. MKONYI	Establishing Youth Platformand participation in goovenance	Citizen's Participation, voice and inclusion	ARUSHA	16,665,000
4	ASSOCIATION FOR TERMINATION OF FEMALE GENITAL MUTILATION (ATFGM) P.O.BOX 431 TARIME : 0784 503126/ 07533326670, STELLA M. MGAYA	Community Empowerment on the elimination of all forms og Gender Based Violence	Citizen's Participation, voice and inclusion	MARA	16,222,500
5	BAGAMOYO WOMEN DEVELOPMENT NETWORK (BAWODENE) - P.O.Box 397 Bagamoyo - 0718 574 587 - Nuru Omari Mhami	Mafunzo ya umuhimu wa wanawake kuhudhuria clinic kwa wakati	Effective Public Service Delivery	PWANI	4,014,300
6	CENTRE FOR ENVIRONMENTAL LAW AND GOVERNANCE LIMITED: P.O.BOX 55919 Dar es salaam; 0785 444 111, Elias Mwashiuya-Executive Director	Countering Gender-supressive traditions in Manyara through Advocacy	Citizen's Participation, voice and inclusion	MANYARA	40,331,737
7	CHAMA CHA ALBINO TANZANIA- TAWI LA WILAYA YA BUKOMBE MKOA WA GEITA - P.O.Box 03 - Bukombe Geita - 0756 287 662 - Emmanuel S Maduka- Mratibu	Mradi wa kampeni na ushawishi kupinga mauaji ya watu wenye ualbino wilaya ya Bukombe mkoa wa Geita	Citizen's Participation, voice and inclusion	GEITA	36,447,500
8	CHAMA CHA UZAZI NA MALEZI BORA TANZANIA (UMATI) - P.O.BOX 2082 ZANZIBAR - 0777495764/0672059420 - SAID SALIM MAALIM- MRATIBU	USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA UENDESHAJI WA SERIKALI ZA SHEHIA	Citizen's Participation, voice and inclusion	UNGUJA	7,568,360
9	CHAMA CHA WALEMAVU TANZANIA LEMELA P.O.Box 3009 MWANZA 0784955415 Msafiri Makoba-Katibu	Kuelimisha watu wenye ulemavu na jamii kuhusu haki za watu wenye ulemavu sambamba na sharia, sera na mkataba wa umoja wa mataifa	Citizen's Participation, voice and inclusion	MWANZA	26,671,900
10	CHAMA CHA WALEMAVU TANZANIA(CHAWATA KAGERA):P.O.Box 1633 Bukoba; 0759 336 331, Consolatha Medard-Mweka hazina	Haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu wa viungo	Citizen's Participation, voice and inclusion	KAGERA	26,473,000
11	CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT) RUKWA BRANCH - P.O.BOX 183 RUKWA - 764727121 - BONIPHACE LAURENT MBALAZI - MEMBER	Raising Awareness and Advocacy for Albino rights	Citizen's participation, Voice and Inclusion	RUKWA	13,260,000
12	CHAWATA MBINGA - S.L.P 194 MBINGA - 764710373 - DENIS NDOMBA-MWENYEKITI	kutoa mafunzo ya sheria no.9 ya mwaka 2010 ya watu wenye ulemavu	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	RUVUMA	8,539,429
13	CHILD SUPPORT TANZANIA:P.O.BOX 1420 Mbeya; 0763 753 353/ 0786 780 706, Noelah Msuya Shawa- Executive Director	Take all my friends to school	Effective Public Service Delivery	MBEYA	25,681,550
14	CHILDREN AND YOUTH DEVELOPMENT CENTRE-CHAYODE - S.L.P 234 MOROGORO - 0754033324 - RAJAB HUSSEIN- MKURUGENZI	ufuatiliaji shirikishi jamii katika matumizi ya rasimali za umma	Accountable Decision Making	MOROGORO	14,417,000
15	CHILDREN'S DIGNITY FORUM(CDF): P.O.Box 34241 Dar es salaam; 0713 691 375/222 775 010, Koshuma Mtengeti- Executive Director	Advancing Girls'Rights-End Child Marriages,Female Genital Mutilation and Empowering Child Mothers in Tarime District, Mara Region	Citizen's Participation, voice and inclusion	MARA	60,823,000
16	COMMUNITY DEVELOPMENT SUPPORT(CDS): P.O.Box 158 Simiyu; 0787 384 612/0753 045 489, Madaraka J.Almasi- Manager	Promotion and protection of persons living with Albinism from violence discrimination and abuse	Citizen's Participation, voice and inclusion	SIMIYU	13,558,300
17	COMMUNITY ECONOMIC DEVELOPMENT & SOCIAL TRANSFORMATION (CEDESOTA) - P.O.BOX 13712 ARUSHA - 0754548180 - JACKSON E.MURO	Women,s Land Rights Project in Meru	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	ARUSHA	11,288,500
18	COMMUNITY FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT(CSD) - P.O.Box 2479 Mwanza - 0764 762 913 - Kulwa Jackson	Ushirikishwaji na uwajibikaji wa wananchi na jamii katika jkupanga bajeti na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali	Accountable Decision Making	MWANZA	11,473,883

19	CONCERN FOR COMMUNITY RESOURCES DEVELOPMENT - P.O BOX 70 KANYIGO MISENYI - 0755779605 - GODWI LUTIMBA CHAIR PERSON	ubunifu wa mbinu shirikishi za misitu ya asili	Citizen's participation, Voice and Inclusion	KAGERA	7,018,500
20	COUNSELLING AND FAMILY LIFE ORGANIZATION(CAFLO): P.O.Box 79039 Dar es salaam; 0682 950 731/0717 977 370, Godfrey Mkoba- Director	Promoting youth rights for sustainable development in good governance	Citizen's Participation, voice and inclusion	DAR ES SALAAM	11,780,000
21	DIRA THEATRE GROUP - P.O.Box 5458Morogoro - 0755 840 581/ 0714 505 195 - Erasmo Emmanuel Tullo-Mkurugenzi	Nafasi ya jamii na viongozi wa vijiji na kata katika utekelezaji wa sera na sheria za ardhi ili kukuza na kulinda Haki ya Umiliki wa Ardhi hasa kwa wanawake	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	MOROGORO	13,798,935
22	DIRA YA MAENDELEO TANZANIA(DIMATA) - P.O.Box 52 Mzumbe, Morogoro - 0713 334 148 - Salum Wamaywa-Katibu	Kujenga uwezo kwa wananchi katika ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za ruzuku za umma katika sekta ya elimu katika kata 10 za wilaya ya mvomero	Effective Public Service Delivery	MOROGORO	13,308,000
23	EQUALITY FOR GROWTH: P.O.Box 10618 Dar es salaam; 0765 447 539/ 222 863 293,Jane Magigita-Executive Director	Enhancing the role of informal sector in promoting good governance and accountability at the local government level: voices of women and men market traders at 6 local markets of the Mwanza Municipal Council	Citizen's Participation, voice and inclusion	MWANZA	63,051,000
24	GEITA REGION NGOs NETWORK BOX 593 GEITA 752818849 MARIUM MKAKA-KATIBU	kujenga uwezo wa kisheria kwa watu wenye ulemavu	Citizen's Participation, voice and inclusion	GEITA	7,185,000
25	GENDER EMPOWERMENT FOUNDATION - P.O.BOX 78970 DAR ES SALAAM - 0754577909/0715577909 - ROSE K. NYONI-MKURUGENZI	Kuyajengea uwezo makundi ya vijana katika manispaa ya kinondoni	Citizen's Participation, voice and inclusion	DAR ES SALAAM	14,293,800
26	HAKI ELIMU: P.O.Box 79401 Dar es salaam; 215185/3, John Kalage-Executive Director	Promoting Accountability and quality of Education	Accountable Decision Making	MANYARA	39,361,803
27	HEALTH ACTIONS PROMOTION ASSOCIATION(HAPA-SINGIDA): P.O.Box 1013, Singida; 262 502 499/0783 306 111, Mwita Kennedy Nyamburi-Executive Director	Strengthening Citizen Participation in planning and budgeting amon local government	Accountable Decision Making	SINGIDA	21,381,760
28	HIGHLANDS HOPE UMBRELLA(HHU): P.O.Box 11 Njombe; 0754 092 365 /0787 759 143, Betty Ludike- Director	Efficiency gains for public health services delivery in Njombe	Effective Public Service Delivery	IRINGA & NJOMBE	24,315,740
29	ILEMELA DISTRICT CSOs NETWORK - S.L.P 6369 Mwanza - 0754/0622/0686-803 114 - Nicas Nibengo- Mwenyekiti	Kukuza ushiriki wa wananchi katika matumizi ya rasilimali za umma -Ilemela	Accountable Decision Making	MWANZA	14,187,600
30	IRINGA CIVIL SOCIETY ORGANIZATIONS (ICISO-UMBRELLA) P.O.BOX 317 IRINGA 0753663282 RAPHAEL M. MTITU- EXECUTIVE SECRETARY	community engagement on improving livehood and government accountability	Citizen's Participation, voice and inclusion	IRINGA & NJOMBE	28,711,667
31	IRINGA DEVELOPMENT OF YOUTHS, DISABLED AND CHILDREN CARE(IYDC): P.O.Box 795 Iringa; 0784 662 224, Johnnie Nkoma-Executive Director	Wanawake kumiliki mali na rasilimali	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	IRINGA & NJOMBE	10,029,722
32	JITAMBUE LEMBUKA TANZANIA(JLT):S.L.P 538 Mbeya; 0755 785 328, Simon Mkanya-Mkurugenzi Mtendaji	Kuimarisha mfumo, miundombinu na uwajibikaji katika sekta ya afya wilayani Kyela	Effective Public Service Delivery	MBEYA	9,355,883
33	JUMUIYA YA KUELIMISHA ATHARI ZA MADAWA YA KULEVYA UKIMWI NA MIMBA KATIKA UMRI MDOGO (JUMAMKUM) - S.L.P 287 CHAKECHAKE -PEMBA - 777150012 - HASSAN ABDALLAH RASHID MWENYEKITI	kuwafkiria na kuwajengea uelewa wanajamii na vijana	Citizen's Participation, voice and inclusion	PEMBA	8,185,000
34	JUMUIYA YA USTAWISHAJI WA ZAO LA KARAFUU NA VIUNGO PEMBA- JUKAVIPE - P.O Box 219 Chake chake - 0777 482 451 - Hassani Ali Bakar- Mratibu	Kuboresha utekelezajiwa sera na sheria za mabaraza ya vijana	Citizen's Participation, voice and inclusion	PEMBA	15,542,000
35	KAGERA CENTRE FOR POVERTY ALLEVIATION - P.O.BOX 738 BUKOBA - 763811800 - SARAPHINA JULIUS - CHAIRPERSON	To promote community participation in public expenditure tracking surveys PETS and Government budget process through lobbying and advocacy	Accountable Decision Making	KAGERA	14,467,060
36	KAGERA DEVELOPMENT AND CREDIT REVOLVING FUND { KADETFU} - P.BOX 466 BUKOBA - 0754740267 - YUSTO PARADIUS MUCHURUZA -EXECUTIVE DIRECTOR	BUILDING CAPACITY OF THE PUBLIC	Accountable Decision Making	KAGERA	6,883,000

37	KILIMANJARO NGO CLUSTER ON STIs, HIV/ AIDS AND RH INTERVENTIONS(KINSHAI): P.O.Box 7445 Moshi; 27-2750747/0754 269 799, Veronica.F.Shayo-Executive Director	Promoting good governance and accountability on water development public funds	Effective Public Service Delivery	KILIMANJARO	18,308,500
38	KILOMBERO GROUP FOR COMMUNITY DEVELOPMENT - P.O.Box 624 Ifakara,Morogoro - 0784 506 388 - Christina Dominic Kulunge-Coordinator	Kutathimini ufanisi wa mgawanyo, mtiririko na matumizi ya mafungu ya fedha elimu ya msingi Kilombero	Accountable Decision Making	MOROGORO	7,494,490
39	LARETOK-LE SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU NGORONGORO (LASHEHABINGO); P.O.BOX 85 LOLIONDO, 0784851434/ 0767851434	Kuimarisha utawala bora na hakiza binadamu kwa wananchi	Citizen's Participation, voice and inclusion	ARUSHA	13,778,000
40	LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE(LIWOPAC): P.O.Box 498 Lindi,0716 503 084,Cosma Bulu- Mkurugenzi	Okoa maisha ya watoto wachanga kwa maendeleo endelevu Lindi	Effective Public Service Delivery	LINDI	36,277,802
41	MATONYOK WOMEN INITIATIVE ORGANIZATION (MWIO) - P.O.BOX 350 Same - 0754566585 - Josephine Nafuna -Director	land Use and Management	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	KILIMANJARO	13,650,304
42	MBARALI WATER SANITATION AND ENVIRONMENTAL CONSERVATION ORGANIZATION (MWECO) - P.O.Box 28 Rujewa-Mbeya - 754503955 - Nikumwitika A. Ngondo-Mwenyekiti	kujenga uwezo kwa jamii juu ya athari na changamoto zinazo wakabili wanawake/ wasichana wa wilaya ya mbarali katika upatikanaji wa huduma za afya na elimu na njia za utatuzi	Effective Public Service Delivery	MBEYA	11,553,940
43	MBEYA NON GOVERNMENTAL ORGANIZATION; P.O.BOX 6404 MBEYA; 0786 792568 SIMON MWANG'ONDA	Uboreshaji wa Utoaji Huduma katika sekta ya Elimu na Afya	Citizen's Participation, voice and inclusion	MBEYA	20,803,724
44	MBEYAB HIV/AIDS NETWORK TANZANIA:P.O.Box 1430Mbeya; 0753 859 262, Jonathan Mwashilindi- Executive Director	Creating youth platform and conducive environment for developmental discussion among youth and holding government accountable in 5 wards of Mbeya Rural district Mbeya region	Citizen's Participation, voice and inclusion	MBEYA	20,409,500
45	MSICHANA INITIATIVE ORGANIZATION:P.O.Box 13355 Dar es salaam; 0762 758281, Rebeca Zakayo Gyumi-Executive Director	Girl empowerment on the issue of child marriage in Bahi Disrict-Dodoma region	Citizen's Participation, voice and inclusion	DODOMA	22,127,100
46	MTANDAO WA ASASI ZA KIRAIA ZA KASKAZINI UNGUJA (NORECSONET) - P.O.BOX 2385, Zanzibar -0777 431 613 - Ali Shauri Ali-Katibu	Kuimarisha ushirikishwaji wa vijana katika sera za kitaifa kupitia mabaraza ya vijana	Citizen's Participation, voice and inclusion	UNGUJA	15,688,000
47	MTANDAO WA MASHIRIKA YASIO YA KISERIKALI WILAYA YA RUANGWA: P.O.Box 33 Ruangwa; 0769 477 635/0718 572 703 Issa Omari Chijuni-Mkurugenzi mtendaji	Kuboresha huduma za wajawazito na watoto wilayani Ruangwa	Effective Public Service Delivery	LINDI	23,111,260
48	MTANDAO WA VIKUNDI VYA WAKULIMA TANZANIA (MVIWATA-RUVUMA) - P.O.BOX 696 SONGEA - 0782879891/ +255 252 600 626 - RAHEL TERRY	stop land grabbing, defend for your life	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	RUVUMA	11,390,080
49	MTWARA DISTRICT NGO NETWORK: S.L.P 318 Mtwara; 0718 819 453, Fidea Amon Ruanda- Katibu mtendaji	Kujenga uwezo na uelewa wa jamii wa ufuatiliaji katika matumizi ya rasilimali za umma(PETS) katika sekta ya Elimu katika halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mkindani	Accountable Decision Making	MTWARA	25,028,672
50	MTWARA PARALEGAL CENTRE COMPANY LIMITED - BOX 247 MTWARA - 0755100266 - MULLOWELLAH ABDALLAH MTENDAH-EXECUTIVE DIRECTOR	Empower community member on land ownership rights and access customary tittle deed	Effective Public Service Delivery	MTWARA	13,220,000
51	NABROHO SOCIETY FOR THE AGED: P.O.Box 299 Busega Simuyu; 0766 940 499, Kubini Nkondo Kubini- Program Manager	People with albinism demanding action(Pewada)	Citizen's Participation, voice and inclusion	SIMIYU	25,975,070
52	NEW AGE FOUNDATION(NAF) ZAMANI TANGA YOUTH DEVELOPMENT ASSOCIATION(TAYODEA): P.O.Box 5344, Tanga; 0713 244 967, David Chanyegea-Mkurugenzi	Ushiriki wa vijana katika kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma	Accountable Decision Making	TANGA	22,174,031
53	NEW LIGHT CHILDREN CENTRE ORGANIZATION-NELICO:P.O.Box 160 Geita; 0767/0784 940 550, Paulina Alex-Executive Director	Dispelling deadly myths and upholding social welfare of people with albinism in 20 wards of Geita District	Citizen's Participation, voice and inclusion	GEITA	23,231,800

54	NYAKITONTO YOUTH FOR DEVELOPMENT TANZANIA: P.O.Box 890; 0765794896 Joel Ramdhan Nkembanyi-Project Coordinator	Participatory Actions for Social Accoutability, Resource management and Fight against Corruption in Kigoma Ujiji	Citizen's Participation, voice and inclusion	KIGOMA	24,495,000
55	RADIO FARAJA: P.O.Box 47, Shinyanga; 0755023472 Anikazi Kumbemba-Assisant Director	Creating awareness about alibinim (CAAA)	Citizen's Participation, voice and inclusion	SHINYANGA	27,639,000
56	ROAD SAFETY AMBASSADORS	Raia paza sauti kuongeza usalama barabarani	Citizen's participation, Voice and Inclusion	DAR ES SALAAM	3,442,000
57	RUFIJI SOCIAL DEVELOPMENT INITIATIVE - P.O.BOX 91 KIBITI RUFUJI - 0783 918985/0717322262 - ALLY MASIMIKE	Uboreshaji wa Elinu ya Sekondary	Effective Public Service Delivery	PWANI	7,142,000
58	SAFARI DEVELOPMENT ORGANIZATION P.O.BOX 2505 ZANZIBAR -P.O.BOX 2505 ZANZIBAR -0777906310 - MWINYI SHABAN SARBOKO	Kuanzishwa kwa Majukwaa ya Vijana	Citizen's Participation, voice and inclusion	UNGUJA	9,968,500
59	SINGIDA INTER-AFRICAN COMMITTEE (SIAC) - P.O.Box 794 Singida - 0755 153 881 - Hadija Juma- Mkurugenzi	Kuwa na jamii iliyo huru kutokana na ukatili wa kijinsia na mila potofu	Citizen's Participation, voice and inclusion	SINGIDA	20,437,812
60	STARVE FOR HELPING OTHER PEOPLE(SHOP) - P.O.Box 1577 Mbeya - Tusekile Agrey-Mwenyekiti	Muungano wa vijana kupitia club katika kujiletea maendeleo	Citizen's Participation, voice and inclusion	MBEYA	15,994,716
61	TAKE SCIENCE FOUNDATION -P.O.BOX 268 LUSHOTO - 0674204976 -GADSON W. HONKONYA	Ufuatiliji wa Bajeti ya sekta ya elimu	Accountable Decision Making	TANGA	12,105,700
62	TANGANYIKA LAW SOCIETY: P.O.Box 2148 Dar es salaam; 0779 626 210, Kaleb Lmeck Gamaya-CEO	Advocacy campiign on the right to information Bill 2016 and police and auxiliary Service Act	Citizen's Participation, voice and inclusion	DAR ES SALAAM	12,564,501
63	TANZANIA ASSOCIATION OF THE DEAF(CHAVITA) NATIONAL HEADQUARTERS:P.O.Box 21591Dar es salaam;0754 670 382/0755 847 764 ,Mr Dickson Francis Mveyange-Executive Director	Improving community attitude towards deaf people and communication skills project	Citizen's participation, Voice and Inclusion	DAR ES SALAAM	15,314,073
64	TANZANIA COUNCIL OF SOCIAL DEVELOPMENT(TACASODE): P.O.Box 63196 Dar es salaam; 0754 284 392, Theofrida Alex Kapinga	Enhancing to Engage with and influence Transparency and accountability in Tanzania	Accountable Decision Making	SINGIDA	57,028,210
65	TANZANIA HUMANI RIGHTS DEFENDERS COALITION: P.O.Box 105926 Dar es salaam; 0783 172 394, Onesmo Olengurumwa-Director	Amplifying the voice of CSOs, Human Rights Defenders and Youth in democritization processes and Policy Management	Citizen's Participation, voice and inclusion	DAR ES SALAAM	13,010,000
66	TANZANIA LEAGUE OF THE BLIND - KWIMBA - TANZANIA LEAGUE OF THE BLIND:P.O.BOX 88 Ngudu Kwimba; 0678 493 548, Salu Kaswahili-Mwenyekiti	Ushawishi na utetezi kwa watu wenye ulemavu kushiriki katika maamuzi kwenye ngazi za umma na kupatiwa haki zao	Citizen's Participation, voice and inclusion	MWANZA	20,963,220
67	TANZANIA LIFE IMPROVEMENT ASSOCIATION(TALIA): P.O.Box 1303 Mtwara; 0762 971 994/0717 390 029, Ayoub Samweli-Mkurugenzi	Kuimarisha uwezo na uwajibikaji wa jamii na viongozi wa serikali katika matumizi ya rasilimali za umma	Accountable Decision Making	MTWARA	20,223,624
68	TANZANIA LIVELIHOOD SKILLS DEVELOPMENT AND ADVOCACY FOUNDATION	Community participation and improved quality of Education	Effective Public Service Delivery	TANGA	22,791,850
69	TANZANIA PEOPLE DEVELOPMENT ORGANIZATION:P.O.Box 346 Bunda Mara; 0768 745 454, George Thomas- Mwenyekiti	Kujenga uwezo wa jamii ili kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana	Citizen's Participation, voice and inclusion	MARA	13,047,500
70	TANZANIA WATER AND ENVIRONMENTAL SANITATION NETWORK(TAWASANET):P.O.Box 33410 Dar es salaam, 0222 462 065, Emmanuel Jackson-National coordinator	Increasing acccountability in the water sector in Kilimanjaro region	Accountable Decision Making	KILIMANJARO	34,459,900
71	THE MAZOMBE MAHENGE DEVELOPMENT ASSOCIATION(MMADEA)	Afya Bora kwa ustawi wa jamii	Effective Public Service Delivery	IRINGA & NJOMBE	23,056,500
72	THE REGISTERED TRUSTEE OF THE ROMAN CATHOLIC DIOCESE OF RULENGE-NGARA: P.O.Box 107 Biharamulo,Kagera; 28 765 753 231, FrHonoratus Ndaula-Executive Secretary	Advocacy for the rights of people with disabilities	Citizen's Participation, voice and inclusion	KAGERA	41,251,458
73	TUMAINI WAVIU NETWORK(TUWANET): P.O.BOX 440 Kyela, Mbeya; 0767 076 015/0715 265 517, Jane Sandube-Mkurugenzi	Kuboresha utoaji elimu ya afya ya uzazi kwa watoto wa kike kwa shule za msingi na sekondari	Effective Public Service Delivery	MBEYA	24,263,200

74	TUSAIDIANE MWALONI KIRUMBA(TMK GROUP): P.O.Box 6237 Mwanza, 0755 068 415, Faustine Rugangila-Mwenyekiti	Kuwajengea uwezo wananchi na viongozi wa vijiji na mitaa juu ya ushirikishwaji wananchi katika mipango ya bajeti na maendeleo katika jamii y wavuvi	Effective Public Service Delivery	MWANZA	10,828,307
75	UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM:P.O.Box 15111Arusha;0787 699 600, Makko John Sinandei-Executive Director	Promoting Pastoralists and Hunter gatherer Women rights of access and ownership of land in Kiteto district	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	MANYARA	42,112,575
76	USHIRIKIANO WA VIJANA MWANDEGE(USHIVIMWA) - P.O.Box 82 Mkuranga Pwani - 0782 290 374 - Mohamedi Omari Mbonde- Mkurugenzi	Elimu ya afya ya uzazi kwa vijana	Effective Public Service Delivery	PWANI	20,500,000
77	VICTORY YOUTH SUPPORT ORGANIZATION - S.L.P 5143 Morogoro - 0765 631831 - Fredrick Ng'atigwa-Mkurugenzi	nafasi ya jamii katika ufuatiliaji wa matumizi ya Rasilimali za umma sekta ya elimu tarafa ya mvua wilaya ya Morogoro Vijijini	Accountable Decision Making	MOROGORO	11,547,500
78	WAJANE WOMEN GROUP (WWG) S.L.P 50106 DAR ES Salaam - S.L.P 50106 DAR ES SALAA - 0712463831 - JANE ANTHONY KIWILI-MWENYEKITI	KUDHIBITI MIMBA KATIKA UMRI MDOGO	Effective Public Service Delivery	DAR ES SALAAM	14,026,000
79	WATAALAM GROUP GAIRO - S.L.P 22 GAIRO - 0654151115 - SALUM H DIBEGA- KATIBU	ufuatiliaji wa rasilimali za umma sekta ya elimu	Accountable Decision Making	MOROGORO	13,285,000
80	WIDOWS AND ORPHANED DEVELOPMENT ORGANIZATION:P.O.Box 79, Geita; Mariam S.Mkaka-Mwenyekiti	Uwazi na Ushirikishwaji wa jamii katika mipango na bajeti za rasilimali za umma	Accountable Decision Making	GEITA	27,839,038
81	WOMEN DEVELOPMENT FOR SCIENCE AND TECHNOLOGY ASSOCIATION(WODSTA): P.O.Box 3182 Arusha; 0754/0784 388 213, Lyne Ukio- Secretary general	Women empowerment through land rights	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	ARUSHA	23,831,899
82	WOMEN POVERTY ALLEVIATION IN TANZANIA; P.O.BOX 3052 MOROGORO, 0715 095565 AMIN M. BAKARI	Women to access land and property rights	Quality of Policy, Legal and Institutional Framework	MOROGORO	48,033,490
83	WOMEN WAKE -UP(WOWAP):P.O.Box 128 Dodoma;0715 786371/0754 562267 Fatma Hassan Toufiq- Chairperson	Addressing Gender Based Violence through reducing prevelance of early Child Marriages among girls in Dodoma region	Citizen's Participation, voice and inclusion	DODOMA	41,485,000
84	WOMEN'S LEGAL AID CENTRE(WLAC): P.O.Box 79212 Dar es salaam; 222 664 051/ 0754 431 699, Theodosia Muhulo-Executive Director	Community legal empowerment for eguality and good governance	Citizen's Participation, voice and inclusion	DAR ES SALAAM	60,170,001
85	WOTE SAWA YOUNG DOMESTIC WORKERS ORGANIZATION: P.O.BOX 10801 Mwanza; 0769 624 323, Angela Benedicto- Executive Director	Kuwa na jamii iliyo huru kutokana na ukatili wa kijinsia na mila potofu	Effective Public Service Delivery	MWANZA	31,502,000
86	ZANZIBAR ASSOCIATION OF INFORMATION AGAINST DRUG ABUSE AND ALCOHOL P.O.Box 615, Zanzibar 0777611133 Masoud Ali Soud-Administrator	Zanzibar Youth voice	Citizen's Participation, voice and inclusion	UNGUJA	9,965,000
87	ZINDUKA DEVELOPMENT INITIATIVE FORUM:P.O.Box 422 Bunda; 0764 211 210, Madoro E.Max-Director	Reducing and mitigating Gender based violence in Bunda District	Citizen's Participation, voice and inclusion	MARA	18,240,864
	SUB TOTAL				**1,838,696,249**

Ofisi Kuu

Mtaa wa Madai Cresent, 7 Ada Estate Kitalu Na. 154. S.L.P. 7192 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255-22-2664890-2 Nukushi: +255-22-2664893

Barua pepe: information@thefoundation-tz.org Tovuti: www.thefoundation.or.tz